# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

## Kikao cha Tano – Tarehe 4 Septemba, 2023

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu changamoto na malalamiko yaliyojikeza Katika kutekeleza Mkataba wa Mauziano ya Matrekta ya Kampuni ya *URSUS* kati ya Shirika la Taifa la Maendeleo *(NDC)* na wakulima kwa utaratibu wa mikopo.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**4 SEPTEMBA, 2023**

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize lake.

Na. 55

**Ubora wa programu mbalimbali zinazotolewa kwa vijana**

**MHE. NG'WASI D. KAMANI** aliuliza:-

Je, Serikali inatumia mfumo gani kuhakiki ubora na matokeo chanya ya programu mbalimbali zinazotolewa kwa vijana?

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Mheshimiwa Patrobass Katambi. Majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya miradi na programu zote zinazotekelezwa ikiwemo programu za vijana. Katika kutekeleza hilo mwezi Januari, 2022 Serikali ilitoa Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Miradi mbalimbali na Programu za Maendeleo. Kwa kuzingatia mwongozo huo, Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu imekuwa ikifanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa programu mbalimbali kila robo mwaka. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu imekuwa ikifanya tafiti ili kupima matokeo ya utekelezaji wa programu mbalimbali,

ikiwemo utafiti wa nguvu kazi ambao hufanyika kila baada ya miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya utafiti wa nguvu kazi uliofanyika mwaka 2020/2021unaonesha kuwa kutokana na programu za vijana zinazotekelezwa ikiwemo Programu ya Kukuza Ujuzi, kiwango cha ujuzi cha juu kimeboreka. Kiwango cha ujuzi cha kati kimeongezeka kutoka asilimia 16.6 mwaka 2014 hadi kufikia asilimia 19.9 mwaka 2021, na kiwango cha ujuzi wa chini kimepungua kutoka asilimia 79.9 mwaka 2014 hadi asilimia 76.9 mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kusimamia utekelezaji wa programu hizo ili ziweze kuleta tija kwa Taifa. Sambamba na hatua hiyo, mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imepanga kufanya tathmini mahususi *(tracer study)* ya mafunzo yanayotolewa kupitia programu mbalimbali za kuwawezesha vijana kubaini mafanikio yaliyopatikana kwa kuwezesha kujiajiri na kuajiriwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, swali la nyongeza.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu ya mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, kwa kuwa lengo kuu la hizi programu ni kutatua changamoto kubwa za vijana ikiwemo kukuza elimu ya ujuzi na kutatua changamoto ya ajira, kumekuwa na changamoto ya vijana wengi ambao wananufaika na hizi programu kushindwa kuunganishwa moja kwa moja na masoko ya ajira na mitaji pale wanapohitimu. Sasa, ni upi utaratibu au mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kuwa vijana hawa wanapohitimu programu hizi wanaunganishwa moja kwa moja na masoko ya ajira au mitaji ili wasirudi mitaani na kuondoa tija ya hizi programu wanazopata?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, bado kuna changamoto ya taarifa hasa kwa vijana wengi waliopo vijijini ya namna gani programu hizi zinapatikana, vigezo na utaratibu wa kuweza

kupata programu hizi. Sasa ni nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha inaboresha mifumo ya taarifa ili vijana wengi wa Tanzania waweze kufahamu fursa hizi na kunufaika nazo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, upo utaratibu ambao Serikali inaendelea nao na tumekuwa tukiendelea kuufuatilia na kufanyia tathimini kuhusu namna ya kuunganishwa na ajira lakini pia kupata fursa za mitaji. Wote tutakuwa mashahidi kuwa kupitia Halmashauri zetu wapo Maafisa Maendeleo ya Vijana lakini pia Maafisa Maendeleo ya jamii. Wote hawa wanaendelea kutoa mafunzo kwa utaratibu wa mwongozo. Mikopo ya asilimia kumi kwanza inatangazwa lakini pili ni takwa la Ilani ya Chama cha Mapinduzi na tatu inaendelea kutangazwa katika Halmashauri zetu zote. Viongozi wengi sana na hata Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakihamasisha uwepo wa ile mikopo ya asilimia kumi. Pia ipo mifuko mingine ya uwezeshaji vijana ukiwemo Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ambao upo Ofisi ya Waziri Mkuu na tumekuwa tunautangaza kupitia Mwenge wa Uhuru.

Mheshimiwa Spika, pia zipo programu nyingine katika wizara za kisekta. Ipo mipango ya kisekta ya kuwasaidia vijana kwa mfano kwenye masuala ya fursa za ajira, kuwaandaa kwenye ajira na mitaji. Pia tuna Wakala wa Ajira *(TaESA)* ambaye ana jukumu kubwa; kwanza la kuwatambua vijana wote wahitimu, pili kuwapeleka kwenye programu mbalimbali ikiwepo utarajali na kuwapeleka kwenye mafunzo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara zote za Kisekta zimekuwa na programu za vijana zinazohusiana na uandaaji wao wa kupata ajira hata ukiangalia Wizara ya Kilimo tunayo *Building a Better Tommorow (BBT)* ambayo ni kwa ajili ya kilimo biashara. Wizara ya

Mifugo na Uvuvi nayo ina programu ambayo ni *BBT Life* ambayo inahusiana na unenepeshaji mifugo.

Mheshimiwa Spika, hao wote wamekuwa wakikutanishwa na masoko ya ajira lakini pia masoko ya malighafi ambazo wanazitengeneza katika maeneo hayo. Nikiongelea la mwisho ambalo ameniuliza kuhusu changamoto za vigezo na taarifa, hili limeelezwa wazi kwenye mwongozo wa utoaji wa mikopo ya asilimia kumi yaani 4:4:2, almaarufu katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, hata sisi kwa upande wa Wizara tumeendelea kufanya hivyo siyo tu katika ufuatiliaji na tathimini lakini pia tumeendelea kutoa elimu kwa vijana na kuitangaza katika maeneo mbalimbali ikiwemo vyombo vya habari, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko miongoni mwa baadhi ya vijana kwamba hizi programu za mendeleo kwa vijana na hasa zile za kwenda nje zinavyotolewa kunakuwa na upendeleo. Sijui Serikali inasemaje kuhusu tatizo hilo ambalo linalalamikiwa sana? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nakuhakikishia kwamba Serikali hii haina upendeleo kabisa. Serikali ya Awamu ya Sita imeweka wazi vigezo vya vijana kuweza kupata fursa hizi. Tumekuwa tukizitangaza kwenye vyombo vya habari, tumekuwa pia tukiwaambia Waheshimiwa Wabunge fursa zilizopo. Kuhusu fursa

za kwenda nje, tumeingia katika *billeteral agreement,* na mikataba ya kuhusiana na namna gani vijana wanaweza kupata fursa za ajira tulishaieleza.

Mheshimiwa Spika, wapo Mawakala wa Ajira za nje ya nchi ambao wamesajiliwa chini ya Ofisi ya Kamishna wa Kazi. Pia kupitia *TaESA* pamoja na *SUGECO* tumekuwa tukitafuta wahitimu wanaofanya vizuri kwenye vyuo vyote vikuu ikiwemo Chuo cha Kilimo *(SUA)*. Wanafunzi ambao wanafanya vizuri kwenye maeneo mbalimbali wanapata fursa za kwenda kufanya masomo nje ya nchi kwa mfano nchini Israel. Sasa hivi wataenda vijana takriban 600 katika programu hizo.

Mheshimiwa Spika, tunachagua vijana ambao wamefanya vizuri na *reccomendation* hii inafanywa kwa usaili kwa kupitia Chuo Kikuu chenyewe na kuangalia yale matokeo ya nani amefanya vizuri. Kwa hiyo, hakuna Mtanzania ambaye anazuiwa kufanya vizuri na yeyote anayefanya vizuri anachukuliwa na Serikali kwa ajili ya kwenda kupata masomo hayo nje ikiwa ni sambamba na kupata fursa mbalimbali kulingana na sifa na vigezo ambavyo vimewekwa kwa mujibu wa sheria bila upendeleo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 56

**Ujenzi wa Stendi ya Arusha kupitia Mradi wa *TACTIC***

**MHE. MRISHO M. GAMBO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa stendi ya kisasa kwenye eneo la *Bondeni City* Jijini Arusha kupitia Mradi wa *TACTIC?*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mbunge wa Jimbo la Arusha Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia mradi wa kuboresha miundombinu katika Majiji, Manispaa na Miji – *TACTIC* awamu ya pili, itatekeleza ujenzi wa stendi kuu ya kisasa ya mabasi katika eneo la *Bondeni City,* masoko mawili pamoja na bustani moja ya mapumziko kwa lengo la kuboresha huduma za kiuchumi na kijamii kwa wananchi wa Jiji la Arusha na maeneo jirani.

Mheshimiwa Spika, kazi ya usanifu imekamilika na taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata mzabuni zinatarajiwa kukamilika mwezi Disemba, 2023. Baada ya taratibu hizo kukamilika, utekelezaji wa ujenzi kwenye maeneo yaliyoainishwa utaanza, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, swali la nyongeza.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri ametuambia kwamba wanatarajia kukamilisha mchakato wa zabuni mwezi Disemba, 2023.

Je, anaweza akatueleza leo kwamba ni lini wana mpango wa kutangaza tenda hii? Maana ili mchakato ukamilike lazima tenda iwe imetangazwa.

Mheshimiwa Spika, swali la pili la nyongeza; Mradi huu wa *TACTIC* mpaka sasa ulishatangaza *tender* kwa ajili ya kujenga barabara za lami za Engo Sheraton, Olasiti pamoja na Oljoro ambapo tunakwenda kujenga stendi. *Tender* ilitangazwa tarehe 27 mwezi Februari, na *deadline* ilikuwa ni tarehe 14 mwezi wa

Nne. Leo miezi mitano imeshapita lakini mkandarasi bado hajakwenda *site*.

Je, ni lini watampeleka mkandarasi *site* ili barabara hizi za lami za Engo Sheraton, Olasiti na Oljoro zianze kujengwa mara moja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza lini tunatangaza tenda hiyo; kama nilivyosema tupo kwenye hatua za utaratibu wa manunuzi na siwezi kuwa *certain* sana kusema lini *exactily* lakini nakuhakikishia tu kwamba *by* Disemba mwaka huu tutakuwa tumekamilisha taratibu zote za manunuzi, na mkandarasi kwenda *site* kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, pili kuhusiana na hii tenda ya ujenzi wa barabara hizi ambazo mpaka sasa zaidi ya miezi minne, mitano mkandarasi hajaenda *site*. Naomba nitumie fursa hii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, TAMISEMI, kutoa maelekezo kwa Meneja wa TARURA Mkoa wa Arusha, lakini pia Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, kwa maana ya Jiji la Arusha, kuhakikisha wanamfuatilia mzabuni huyo kwa maana ya mkandarasi huyo aanze kazi mara moja kwa kufuata taratibu. Kama kuna mkwamo wowote Ofisi ya Rais- TAMISEMI tutaingilia kati kuhakikisha tunakwamua na kazi inaendelea, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri unaonaje hilo agizo lako lingeenda kwa mameneja wote ambao mradi huo wa *TACTIC* unaenda?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika,

napokea na naomba niseme kuwa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri naelekeza kwa Mameneja wote wa *TARURA* katika mikoa na wilaya ambazo zinatekeleza Mradi wa *TACTIC* kuhakikisha kuwa wanasimamia kwa karibu hatua zote za manunuzi, lakini pia kuhakikisha kuwa wakandarasi wanafika *site* kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa miradi hiyo mara moja. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, swali la nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi nulize swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga Soko na Stendi ya Kisongo Mateves ambayo ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Noah Saputu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali imeweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba, kwanza Halmashauri zenye miradi hiyo zinaainisha gharama zinazohitajika kwa ajili ya ujenzi wa stendi na masoko hayo. Pia, kutenga fedha kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya kuanza utekelezaji. Lakini kama gharama ni kubwa kuliko uwezo wa halmashauri, kuwasilisha Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, tutaenda kulitekeleza hilo, na hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais lazima tutaitekeleza na tutaipa kipaumbele katika miradi yetu ya ujenzi wa masoko na stendi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Samweli Hhayuma, swali la nyongeza.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi; ujenzi wa stendi Mji Mdogo wa Katesh unasuasua; je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kuwa stendi hiyo inakamilika haraka ili ianze kutumika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa *Engineer* Hhayuma, Mbunge wa Jimbo la Hanang kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, natoa maelekezo na nasisitiza kwa Mkurugenzi wa Halmashauri hii ya Hanang. Tulishafanya ziara pale, mimi na Mheshimiwa Mbunge lakini pia tuliona kweli stendi ile inasuasua. Tulitoa maelekezo na Halmashauri ilitoa *commitment* ya kuongeza fedha kwa ajili ya kukamilisha. Kwa hiyo, tunatoa maelekezo kwamba wahakikishe wanakamilisha stendi ile haraka iwezekanavyo na sisi Ofisi ya Rais-TAMISEMI tutafika kukagua na kuona kazi imetekelezwa kwa wakati, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa John Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itaanza upya mchakato wa ujenzi wa stendi ya kisasa eneo la Madira, mchakato huo ambao ulisitishwa mwaka 2019 ghafla wakati umefikia hatua ya utekelezaji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, naomba nilichukue hili suala la stendi hii ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja kule Arumeru tuone kwa nini ilisitishwa ghafla mwaka 2019, na hatua zipi zimechukuliwa kuondoa changamoto hiyo ili lengo la Serikali kuwahudumia wananchi kwa kujenga stendi hiyo liweze kukamilika kwa wakati.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri ili tukomboe wakati, Mbunge nakuwa nimeshamwita mimi nimemtaja kwa hiyo, huna haja ya kumtaja tena ili tupunguze matumizi ya muda. Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Swali langu ni katika miji ile 45 na Makambako ipo; je, ni lini Serikali itaanza kujenga stendi na soko kwa Mji wa Makambako?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza Mradi wa *TACTIC* katika Halmashauri ya Mji wa Makambako. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, nafahamu Makambako ipo awamu ya pili au ya tatu. Tunakwenda kusukuma kuhakikisha ujenzi wa stendi na soko katika Mji wa Makambako unaanza mapema iwezekanavyo. Najua taratibu za usanifu zimeshafanyika na zinaendelea kukamilishwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, swali la nyongeza.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante, je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa stendi ya mabasi katika Mji wa Babati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika,

stendi ya mabasi katika Mji wa Babati ni kipaumbele cha Serikali na tulielekeza Halmashauri ya Wilaya ya Babati na Halmashauri ya Mji wa Babati zianze kuandaa na anafahamu, Halmashauri ya Mji wa Babati iko kwenye mpango wa *TACTIC*, na mpango huo wa *TACTIC* unaendelea kutekelezwa kama nilivyojibu kwenye majibu yangu ya msingi kwamba tunakwenda kwa awamu ya kwanza, ya pili na ya tatu na sasa zinakwenda sambamba kwa kufuatana. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Halmashauri ya Mji wa Babati ipo kwenye *TACTIC,* lakini kuhusu Halmashauri ya Wilaya ya Babati tutaendelea kuhakikisha kwamba Halmashauri inatenga lakini pia na sisi Serikali Kuu tunaona uwezekano wa ku-*support*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Suma Ikenda, swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mbeya ni Jiji, lakini hauna stendi yenye hadhi ya jiji. Sasa je, ni lini Serikali itajenga stendi Mkoa wa Mbeya? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. NDUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mkoa wa Mbeya ni Jiji na jiji lile kwa bahati nzuri Mbunge wake ni Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson ambaye ni Spika wa Mbunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Serikali inatambua na imeweka kipaumbele kuhakikisha kwamba tunajenga stendi ya kisasa inayoendana na Jiji la Mbeya, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe, ukiwa unataka swali la nyongeza anaposimama mwenye swali la msingi, unasimama na wewe. Maana huwa idadi yenu inaanza kuongezeka kadri tunavyoenda mwisho. Sasa inaniwia ngumu kupanga hapa kwamba watu wangapi naweza kuwaita. Nimewaona wengine wawili mmesimama lakini ni kama vile yaani mlikuwa mnasikilizia hivi.

Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, Halmashauri ya Wilaya wa Kilwa inaendelea na ujenzi wa Stendi ya Mabasi pale Nangurukuru, lakini uwezeshaji wake wa kimapato ni mdogo. Je, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI, iko tayari sasa kuipa fedha Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ili ikamilishe ujenzi wa stendi pale Nangurukuru? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. NDUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ujenzi wa stendi ya mabasi Nangurukuru, ni kweli umeanza kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa. Naomba nitumie fursa hii kusisitiza kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kilwa, kuhakikisha kwamba anaweka kipaumbele kwenye bajeti ya mapato ya ndani kuongeza kasi ya ujenzi wa stendi ile, lakini na sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tutafanya tathmini kuona kama wanashindwa, kwa maana ya uwezo wa mapato kukamilisha kwa wakati ili tuone uwezekano wa kupata fedha kwa ajili ya kuwa-*support* ili kuikamilisha kwa wakati, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Shamsia, swali la nyongeza.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii; je, ni lini sasa Serikali itajenga Stendi na Soko katika Halmashauri yangu ya Wilaya ya Mtwara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. NDUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ujenzi wa stendi na soko katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara ni moja ya mahitaji ya wananchi na Serikali yetu ya Awamu ya Sita imeweka kipaumbele kusogeza huduma za kijamii kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, sasa nitumie fursa hii pia kuendelea kusisitiza kwamba ni wajibu wa Wakurugenzi wa Halmashauri husika kuweka vipaumbele kupitia mapato ya ndani, kuanza

ujenzi wa stendi na soko. Halmashauri zetu nyingi zina uwezo wa kufanya hivyo zikiweka kipaumbele, lakini na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa maana ya Serikali Kuu tutaendelea kufanya tathmini na kuona maeneo ambayo yanahitaji kuongezewa nguvu, tutafanya hivyo ili stendi hizo na masoko yaweze kukamilika kwa wakati, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mbunge wa Morogoro Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 57

### *TARURA* kuongezewa fedha za kukarabati barabara za Morogoro Kusini

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaiongezea fedha *TARURA* kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Jimbo la Morogoro Kusini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. NDUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mbunge wa Jimbo la Morogoro Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TARURA* imeendelea kuongeza bajeti kwa ajili ya ujenzi, ukarabati na matengenezo ya miundombinu ya barabara katika Jimbo la Morogoro Kusini. Bajeti ya utekelezaji wa miundombinu ya barabara imeongezeka kutoka kilometa 51.5 kwa shilingi milioni 660.95 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 hadi kilometa 65.90 kwa shilingi bilioni 1.88 kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya shilingi bilioni 2.2 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi, ukarabati na matengenezo ya miundombinu ya barabara yenye urefu wa kilometa 85.9. Serikali itaendelea kuongeza bajeti kwa ajili ya uimarishaji wa miundombinu ya barabara katika Jimbo la Morogoro Kusini, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Kalogeris, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali, pamoja na Serikali kuendelea kutenga fedha nyingi kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya barabara katika Jimbo la Morogoro Kusini, bado kuna uhitaji mkubwa wa fedha ambazo ningependa Serikali itenge.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kwenda na mimi akaangalie mazingira ya barabara katika Jimbo la Morogoro Kusini ili iwe rahisi kwa Serikali kuendelea kutenga fedha? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. NDUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua kwamba Jimbo la Morogoro Kusini linahitaji fedha zaidi kwa ajili ya utekelezaji wa barabara hizi. Ndiyo maana katika kipindi cha miaka ya fedha mitatu mfululizo, Serikali imeendelea kuongeza bajeti ya barabara katika jimbo hili lakini pia katika majimbo yote.

Mheshimiwa Spika, namhakikishia kwamba nipo tayari kuambatana naye kwenda katika Jimbo la Morogoro Kusini. Tutakubaliana baada ya maswali haya ili tupange, baada ya Bunge tuweze kwenda na kuona hali ilivyo, lakini pia kushirikiana katika kuboresha huduma hiyo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, barabara za Jimbo la Kilwa Kaskazini zilizo nyingi zina hali ya miinuko mikali pamoja na udongo korofi na zina hali mbaya sana. Je, Serikali ina mkakati gani wa barabara za aina hii ili kuboresha na kuhakikisha kwamba zinapitika muda wote wa mwaka? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. NDUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya tathmini ya namna ya kufanya *allocation* ya fedha za barabara kwenye majimbo. Kwa sababu tunafahamu kwamba hali ya hewa inatofautiana, kuna majimbo yenye mvua nyingi kwa mwaka mzima. Kuna majimbo yenye milima na miteremko mikali, lakini kuna majimbo au wilaya ambazo zina udongo korofi kwa ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hata ule mgao wa fedha za Bajeti ya *TARURA* zinakwenda kwa kuzingatia vigezo hivyo, ukiwepo ukubwa lakini na hali ya kijiografia ya maeneo hayo. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, Serikali inatambua kwamba Kilwa Kusini na Kilwa kwa ujumla ina changamoto hiyo na ndiyo maana inaendelea kuongeza bajeti na tutaendelea kufanya hivyo kuhakikisha kwamba barabara hizi zinapitika vizuri zaidi. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Mwanyika, swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, pamoja na maelezo aliyoyatoa sasa hivi, kulikuwa na ahadi ya Serikali kwamba majimbo yale ya mjini, ambayo yana mjini na vijijini yatapewa bajeti kubwa zaidi upande wa *TARURA*. Nini kauli ya Serikali kuhusu kutekeleza azma hiyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. NDUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli ilikuwa ni ahadi ya Serikali na niseme ahadi hiyo imeanza kutekelezwa. Kwa maana ya Manispaa na miji ambayo ina hali ya miji lakini pia vijijini, Serikali imeendelea kuongeza bajeti kuwezesha barabara za vijijini zijengwe vizuri, pia na barabara za mijini zijengwe vizuri.

Mheshimiwa Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge likiwepo Jimbo la Njombe Mjini, tutahakikisha tunaendelea kuboresha utaratibu huu, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, napenda kujua ni lini Serikali itajenga daraja la kuunganisha Kata ya Matongo na Kata ya Kibasuka, Nyarwana ili kusaidia mawasiliano wakati wa mvua? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. NDUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kumwelekeza Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Mara, lakini pia Wilaya ya Tarime kwenda kufanya tathmini ya gharama zinazohitajika katika ujenzi wa daraja hili la Matongo linalounganisha upande wa pili, ili sasa Serikali ifanye tathmini kuona kama liko ndani ya uwezo wa bajeti ya kila mwaka au linahitaji *special* bajeti ili tuweze kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Liwale ndiyo wilaya pekee yenye kilometa chache sana za barabara za changarawe na tuna chini ya kilometa nne tu za lami. Je, Serikali

haioni umuhimu wa kuiongezea wilaya hii fedha za *TARURA* ili kuongeza ufanisi wa ujenzi wa barabara hizo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. NDUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli Jimbo la Liwale lina changamoto kubwa ya barabara. Katika bajeti zetu za miaka mitatu mfululizo, Mheshimiwa Kuchauka ni shahidi kwamba bajeti imeendelea kuongezeka, lakini najua bado haitoshelezi kutokana na ukubwa na changamoto kubwa ya barabara.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kuboresha suala la kuhakikisha kwamba barabara hizo zinatengewa fedha zaidi ili ziweze kupitika vizuri zaidi, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Mji wa Iringa ni mji ambao barabara kubwa zote zinapita katikati ya mji; je, ni namna gani Serikali itatusaidia kwa dharura ili kupanua barabara za pembeni kwa kuwaongezea *TARURA* bajeti?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. NDUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali lengo lake ni kuhahikisha kwamba barabara zetu zinapitika vizuri zaidi. Pia ni jukumu la halmashauri kuainisha maeneo ambayo wanadhani ni muhimu barabara zipanuliwe vizuri zaidi. Mameneja wa *TARURA* wa Mkoa na Wilaya wanatakiwa kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitumie fursa hii kutoa wito kwa Meneja wa *TARURA* Mkoa wa Iringa, wa Wilaya ya Iringa na

Mkurugenzi wa Manispaa ya Iringa, kuainisha barabara hizo, kutambua gharama zinazohitajika ili tuweze kuweka mpango kazi wa utekelezaji kwa awamu, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicodemas Maganga, swali la nyongeza.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Halmashauri ya Wilaya ya Mbongwe imepakana na wilaya nne, lakini bajeti ya *TARURA* haitoshi na barabara zinahitaji kufunguliwa.

Je, ni lini Serikali Kuu itatoa pesa kwa *TARURA* ili kusudi njia zinazounganishwa na Wilaya ya Mbongwe ziweze kufunguliwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. NDUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunatambua Wilaya ya Mbongwe inapakana na halmashauri *almost* nne. Kuna changamoto ya baadhi ya barabara ambazo zinaunganisha Halmashauri ya Mbongwe na halmashauri za jirani. Serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunaboresha ujenzi wa barabara hizo na tutaendelea kufanya hivyo. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, kikao cha Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mameneja wa *TARURA*, aliagiza Mikoa ya Kusini hususan Njombe, ikiwemo Wilaya ya Makete kuangaliwa kwa jicho la karibu kutokana na kwamba ni wilaya ambazo mvua zinanyesha kwa muda mrefu na Makete bajeti ya *TARURA* ni ndogo sana. Je, ni lini Serikali itaongeza fedha hizi na kuzingatia maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. NDUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli yalikuwa ni maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, na sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI kazi yetu ni kutekeleza maelekezo hayo. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tumeshafanya tathmini ya halmashauri zenye mvua nyingi, milima na aina ya udongo ikiwemo Halmashauri ya Makete na bajeti ya barabara katika Halamashauri ya Wilaya ya Makete itaendelea kuongezwa. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Nyamagana, sasa aulize swali lake. Mbunge kutoka Mwanza, Mbunge wa…

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika,…

**SPIKA:** Subiri kwanza Mheshimiwa. Mheshimiwa Joseph Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, kwa niaba ya Mheshimiwa Mbunge wa Nyamagana.

Na. 58

**Ujenzi wa Barabara ya Mkuyuni hadi Mhandu – Mwanza**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI K.n.y. MHE. STANSLAUS S. MABULA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga barabara ya Mkuyuni hadi Mahandu kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. NDUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Jimbo la Nyamagana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mkuyuni hadi Mahandu ina urefu wa kilometa 10.5. Serikali imekamilisha usanifu kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami ambapo kiasi cha shilingi bilioni 20 zinahitajika. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali ilitenga shilingi billioni 5.36 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya urefu wa kilometa 5.04 kiwango cha lami; kilometa 1.725 kiwango cha zege; kilometa 1.8 kiwango cha changarawe; na kilometa 0.7 kiwango cha mawe.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali imetenga shilingi bilioni 3.42 kwa ajili ya ujenzi wa barabara kilometa 2.2 kiwango cha lami; kilometa 1.0 kiwango cha zege; kilometa 6.29 kwa kiwango cha changarawe; na kilometa 2.0 kiwango cha mawe.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuweka kwenye mpango Barabara ya Mkuyuni hadi Mahandu na barabara nyingine katika Jimbo la Nyamagana kwa kutenga bajeti kwa ajili wa ujenzi na matengenezo ya barabara hizo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa miradi mingi inayotekelezwa na *TARURA,* kumekuwa na changamoto ya ubora wa wakandarasi wanaotekeleza miradi hii.

Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha katika miradi hii, pamoja na Serikali kutenga pesa nyingi lakini wakandarasi wanaopatikana wawe na ubora wa kuhakikisha barabara zile zinakuwa vizuri?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwenye Jimbo la Ukerewe barabara inayounganisha Kata ya Nkilinzya na Kata ya Bukindo kuna daraja pale linaleta shida kubwa sana. Je, ni lini Serikali itatusaidia kupata pesa za kujenga daraja linalounganisha Kata ya Bukindo na Kata ya Nkilizya? Nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. NDUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue fursa hii kusisitiza kwa Mameneja wote wa *TARURA* wa Mikoa na Wilaya, kwamba Serikali ilikwishatoa maelekezo kwamba kila tunapotekeleza miradi ya Barabara, kwanza lazima tupate wakandarasi wenye sifa na uwezo wa kujenga barabara kwa kuzingatia ubora na thamani ya fedha, lakini kukamilisha kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, pili, tulishaelekeza kuchukua hatua kwa wakati kwa wakandarasi ambao wataonesha kutokuwa na uwezo mzuri wa kujenga barabara hizo. Pia, kuhakikisha kwamba ikiwezekana tunavunja mikataba hiyo kwa kufuata taratibu za kisheria na kupata wakandarasi ambao wana sifa hiyo. Kwa hiyo, naomba nisisitize kwenye eneo hili, kwamba ni wajibu wa Mameneja wa Mikoa, pia wa Wilaya lakini na halmashauri zetu na Mabaraza ya Madiwani kuhakikisha kwamba wanajiridhisha na ubora wa barabara kabla mradi haujakamilika.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusiana na daraja linalounganisha Kata ya Bukindo na Nkilizya ambalo liko katika halmashauri ya Ukerewe, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunahitaji kufanya tathmini na hivyo meneja wa *TARURA* Wilaya afanye tathmini, watuletee gharama. Tutaona kama Serikali Kuu inahitaji kutoa fedha ama mapato ya ndani yanaweza kujenga daraja hilo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuena Bushiri, swali la nyongeza.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Daraja la Makulu Villa ni daraja linalounganisha Wilaya ya Simanjiro na Wilaya ya Same, lakini daraja hili limekuwa na changamoto kubwa kwa kuwa wakulima na wafugaji wanashindwa kufanya biashara zao. Je, Serikali imejipanga vipi katika kujenga daraja hili ili kuwasaidia wananchi hawa? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. NDUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kuhusu Daraja la Makulu Villa ambalo linaunganisha Halmashauri ya Simanjiro na Same kwamba ni changamoto na linakwamisha shughuli za kiuchumi kwa wananchi, wakulima na wafugaji, naomba Serikali tulichukue hili na tutafanya tathmini kuona uwezekano wa kuweka mpango kwa ajili ya ujenzi au ukarabati wa daraja hilo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali mafupi na maswali yasihusishe uchangiaji wa hoja. Maswali mafupi. Mheshimiwa Dkt. Mathayo David Mathayo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Spika, barabara za milimani zinapowekewa kifusi, mvua inavyonyesha kifusi kinazolewa kwa hiyo Serikali inapoteza fedha nyingi sana. Je, ni lini Serikali itaweka zege katika barabara ya Chome – Tae na Yavumali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. NDUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba barabara za milimani kwa kweli tukizijenga kwa kifusi mara nyingi baada ya msimu wa mvua barabara zinaharibika kabisa na hivyo thamani ya fedha inapotea na ndiyo maana Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia *TARURA* tumefanya tathmini ya aina ya barabara kulingana na hali ya kijiografia ya maeneo husika ikiwemo Halmashauri ya Same, ambayo ina milima mingi.

Mheshimiwa Spika, moja ya *solution* ambayo tumeitafuta, ni kuanza kujenga barabara hizo kwa kutumia mawe. Kwa sababu mara nyingi maeneo yenye miinuko yana mawe pia, lakini pili kutumia zege. Kwa hiyo, kwa hizi barabara ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja, naomba tuzichukue, tufanye tathmini, halafu

tuone uwezekano wa kujenga kwa kiwango cha changarawe, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Mji wa Bunda ni mji unaokua. Serikali iliahidi kujenga barabara za mitaa kwa kiwango cha lami; je, ni lini sasa Serikali itahakikisha inajenga kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. NDUGANGE):** Mheshimiwa Spika, barabara za lami katika Halmashauri ya Mji wa Bunda ni jambo la msingi na Serikali ilishaahidi na imeshaanza utekelezaji kwa awamu. Najua kuna barabara za lami pale zinaunganisha mitaa, lakini nafahamu kwamba kuna uhitaji mkubwa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuhakikisha kwamba tunajenga barabara za lami kwa kadri ya mahitaji ya Mji wa Bunda, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Edwin Swalle, swali la nyongeza.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi. Mji wa Mtwango, Jimbo la Lupembe ni eneo ambalo linakua kwa kasi sana. Serikali ina mpango gani wa kujenga lami katika eneo la Mtwango na barabara ya kwenda Ikuna? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika naomba kujibu swali la uhitaji wa barabara ya lami katika Mji wa Mtwango ambao unaunganisha Ikuna na Mtwango.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mji wa Mtwango unakua kwa haraka sana lakini tulishaelekeza Meneja wa *TARURA* kuweka vipaumbele vya ujenzi wa barabara za lami, katika Halmashauri

zetu zote katika zile fedha za Bajeti za *TARURA* tulielekeza kwamba angalau kuwe na kipaumbele cha kuanza ujenzi wa barabara za lami.

Mheshimiwa Spika, naomba nisisitize kwamba Meneja wa *TARURA* Wilaya ya Njombe asimamie maelekezo hayo, lakini kama fedha ile ya bajeti haitoshelezi afanye tathmini na kuleta Ofisi ya Rais, TAMISEMI tuweze kuona uwezekano wa kupata fedha zingine kwa ajili ya kuongeza nguvu ya utekelezaji wa mradi huo, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Justin Nyamoga, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Ilula kwenda Image - Igumu ipo katika mpango wa kujengwa lami kupitia mradi wa *RISE*. Je, ni lini barabara hiyo itaanza kujengwa ili wananchi wapate barabara bora, kwa sababu barabara hiyo sasa hivi ipo katika hali mbaya sana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Mpango wa *RISE* unaendelea kutekelezwa, ni kweli kwamba barabara hii ya Ilula - Image na Igumu ambayo ameitaja Mheshimiwa Mbunge ziko kwenye mpango huu wa *RISE,* nimhakikishie kwamba mpango ule unaendelea kutekelezwa na muda utakapofika tutahakikisha kwamba barabara hizo kwa kadri tulivyojipangia mpangokazi, zinatekelezwa kwa kiwango hicho ambacho kimepangwa kwenye mpango wetu. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, barabara ya Himo - Sokoni kwenda Lotima ina kilometa 7.5

na Mheshimiwa Waziri Mkuu aliagiza kwamba *TARURA* waweze kuijenga kwa kiwango cha lami na mmeanza mmejenga mita 800 tu.

Je, mnatoa kauli gani kuhusu kumalizia barabara hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nimhakikishie kwamba ni kweli maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali imekwishaanza kutekeleza kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema, tumeanza na mita 800 lakini tunafahamu barabara ile ina urefu wa kilometa 7.5 tutakwenda kwa awamu, safari ni hatua tumeanza, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kuweka kipaumbele kuhakikisha kilometa hizo 7.5 zinajengwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaenda Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, Mbunge wa Kiteto, sasa aulize swali lake.

Na. 59

**Kuongeza kigezo cha kujitolea katika Utumishi wa Umma**

**MHE. EDWARD O. KISAU** aliuliza: -

Je, lini Serikali italeta marekebisho ya Sheria ya Ajira ya Utumishi wa Umma kuongeza kigezo cha kujitolea ili kutoa fursa kwa wanaojitolea?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, Mbunge wa Kiteto, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa sasa inafanya mapitio ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura Na. 298, Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma, Toleo la Pili la mwaka 2008, Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022 na Miongozo inayohusu masuala mbalimbali likiwemo suala la ajira.

Mheshimiwa Spika, endapo itabainika bayana kigezo cha kujitolea kitatakiwa kuingizwa katika marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Serikali italeta Marekebisho ya Muswada wa Sheria Bungeni kwako. Kwa sasa Serikali imeandaa mwongozo unaoweka mazingira wezeshi kwa vijana wanaohitimu katika vyuo mbalimbali kujitolea katika Taasisi za Umma kwa lengo la kuwawezesha kujipatia uzoefu utakaomuwezesha katika ushindani pindi nafasi mbalimbali zitakapotangazwa.

Mheshimiwa Spika, mwongozo huu unalenga kuziba ombwe lililopo kutokana na kutokuwa na utaratibu mmoja ndani ya Taasisi za Umma kuhusu kujitolea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Edward Olekekaita, swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi na nashukuru kwa majibu ya Serikali lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, kwa kuwa kila kazi inayotangazwa tunaambiwa tunataka uzoefu na hakuna mtu anatoka shuleni na uzoefu. Kwa hivyo, walimu wanaojitolea hicho ni kigezo kwamba kujitolea sasa imefika wakati hii sheria iwe ni kigezo namba mbili baada ya *meritocracy*.

Swali la pili, kwa kuwa Wizara nyingi sasa zimeshatengeneza miongozo ya kujitolea, nilikuwa nasoma moongozo wa Wizara ya Elimu wa kujitolea kwa Walimu wa June na Wizara ya Maendeleo ya Jamii wa 2021, kwa nini sasa ninyi ambao ni wa Utumishi, muendelee kupoteza muda badala ya kuleta mabadiliko ya sheria haraka sana? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba iko miongozo mbalimbali ambayo inaongoza juu ya jambo zima la kujitolea, lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako kwamba maagizo yalikwishatolewa na Bunge lako juu ya Serikali kuanza utaratibu wa kuja na sheria na miongozo juu ya jambo la kujitolea kama nilivyoeleza katika jibu la msingi kwamba, kumekuwa na miongozo mbalimbali lakini hakuna utaratibu maalum unaolenga kuelekeza juu ya jambo zima la kujitolea.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako kwamba maagizo uliyoyatoa tunayafanyia kazi, na ndani ya Ofisi ya Rais – Utumishi, tumekwishaanza michakato hiyo na sasa hivi tuko katika *document* na kama nilivyoeleza kwamba *document* zitakapokuwa tayari tutazileta mbele ya Bunge lako Mheshimiwa Spika ili Wabunge waweze kutoa mawazo yao, baada ya hapo sasa tuweze kuleta ije kuwa sheria.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo pia nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako kwamba Serikali inayachukua mawazo yote mazuri yaliyotolewa na Wabunge, pamoja na michango yao katika kipindi cha Bunge la Bajeti na kwamba tunayafanyia kazi na kuyaleta mbele ya Bunge lako ikiwa kama miongozo ya Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa, wako watanzania wengi ambao wana ujuzi na stadi

mbalimbali na ziko nchi ambazo tunapakana nazo zina uhaba wa kada mbalimbali za utumishi.

Je, Wizara hii iko tayari kuketi na Wizara ya Mambo ya Nje ili kuweza kuwasaidia Watanzania hawa waweze kupata ajira katika nchi hizo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, wazo lililotolewa na Mheshimiwa Mbunge la kuketi na Wizara ya Mambo ya Nje, sisi kama Serikali niseme tunalichukua na tutakaa na wenzetu na kutengeneze miongozo mizuri ya kuona ni jinsi gani tunauza ajira nje ya nchi yetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, je, Serikali haioni uko umuhimu sasa wa kuweka majina ndani ya *data base* waliojitolea na wanaoendelea kujitolea ili wawe wa kwanza kuajiriwa wakati huo? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, hali ilivyo kwa sasa na miongozo iliyotolewa na Serikali inahifadhi majina ya watu wote wanaoshiriki michakato mbalimbali inayohusu ajira ndani ya *database*.

Mheshimiwa Spika, nataka nilihakikishie Bunge lako kwamba *database* tuliyonayo sasa inaishi kwa mwaka mmoja, baada ya mwaka mmoja ili turuhusu watu wengine nao waweze kuingia, lakini wazo analolisema ni moja ya mabadiliko makubwa ambayo yanakuja kuletwa na huu mchakato ambao sasa unafanyika wa mabadiliko ya Sheria ya Utumishi, pia sera mbalimbali zilizopo ili kuweza kuweka mahitaji yote ya ajira katika chombo kimoja lakini

mwongozo mmoja ambao utaweza kutoa nafasi kwa Watanzania wote. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba, swali la nyongeza.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Spika ahsante. Msingi wa kuanzishwa kwa mafunzo kwa vitendo kazini ni kuziba ombwe kati ya mafunzo waliyopata wahitimu vyuoni pamoja na soko la ajira. Sasa, kwa kutokuwa na kipaumbele cha kuajiri wale waliopata haya mafunzo kwa vitendo kazini kwanza, ni sawasawa na kupoteza lengo la kuanzishwa kwa mafunzo hayo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri alitaka kumalizia pale mwisho na kuweka kiulizo, kwa hiyo ameweka. *(Makofi)*

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Sasa, kwa kutokuwa na kipaumbele cha kuajiri wale waliopata haya mafunzo kwa vitendo kazini kwanza, ni sawasawa na kupoteza lengo la kuanzishwa kwa mafunzo hayo? *(Makofi)*

*(Hapa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto M. Biteko aliingia Ukumbini na Wabunge walimpigia makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana kwa ukaribisho huo wa heshima, lakini tutamkaribisha rasmi.

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Zainab Katimba niruhusu kidogo na mimi nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ridhiwani huko ni kupoka madaraka sasa, endelea *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nisamehe kwa sababu niliona kwamba niombe ruhusa kwako, nadhani ujumbe umeshafika. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Subiri na wewe umeweka historia, kwa hiyo, nimekuruhusu toa salamu zako. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, sasa naomba nijibu swali la Mheshimiwa Zainab Katimba kuwa ni kweli anayoyasema Mheshimiwa Zainab Katimba na ndiyo maana nataka nikiri mbele ya Bunge lako, wakati wa mijadala mingi inayoendelea juu ya masuala mazima ya ajira na utumishi, jambo la mazoezi ya kujitolea au mafunzo ya vitendo limekuwa ni moja ya jambo la mjadala mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako limesema kwa sauti kubwa na Serikali imesikia. Ndiyo maana sasa tuko katika mchakato wa kufanya *review* ya Sheria yetu ya Utumishi wa Umma ili kuweza kuangalia mapungufu yote yaliyopo na kama nilivyosema kwenye ahadi yetu kwamba tutakapokuwa tayari tutaileta hapa na Bunge lako litapata nafasi ya kutoa mawazo na sisi kama Serikali tuweze sasa kutengeneza sheria ambayo itakuwa inabadilisha Sheria ya Utumishi wa Umma ili kuweza kutengeneza mustakabali mzima wa ajira na vipaumbele katika nchi yetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako, lakini la ujumla nadhani katika kipindi hiki cha kusubiri, wakati Serikali mkijipanga, maadam wapo hizo kada mbalimbali za watu wanaojitolea kwenye hayo maeneo, mtafute utaratibu wa muda ama wa mpito wa kuwatazama hao wakati mnasubiri kufanya hayo marekebisho makubwa. Kwa sasabu wako kule bado wanaendelea kujitolea. Kwa hiyo, nadhani ndiyo maana maswali yanaendelea kujitokeza pamoja na jibu la msingi kusema kwamba Serikali inafanya utaratibu mzuri ili kushughulika na hilo jambo kwa ujumla wake.

Katika hiki kipindi cha mpito ndiyo Serikali itafute namna, ndiyo maana maswali yanaendelea kujirejea kwa sababu wale watu bado wapo kule na hawapewi kipaumbele katika ajira. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika tunalichukua hilo, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na ninamshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu aliyoyatoa, lakini kwa sababu umeweka msisitizo katika jambo hili na Waheshimiwa Wabunge wengi wameuliza, nami ninadhani nitoe kauli kwenye jambo hili kwa sababu ya uzito wake.

Mheshimiwa Spika, wataalam wanafanyia kazi kama tulivyoahidi wakati wa Bunge la Bajeti, nilisema hapa kwamba haiwezekani hatuna Walimu wa hesabu, halafu Walimu wa hesabu wanaendesha bodaboda. Hatuna madaktari halafu madaktari wanalima matikiti hilo haliwezekani, kwa sababu hawa watu wamesomeshwa na rasilimali za nchi na hii ni rasilimali kabisa ipo. Hatuwezi kuwa tuna watu kwa sababu hatuwezi kuwalipa mshahara tukawa hatuna utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niseme tu tunamalizia kuweka huu utaratibu na muda siyo mrefu tutawashirikisha Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu kujitolea huku pia kuna gharama, lazima mtu apate huduma za msingi. Kwa hiyo, kuna *cost implication* lazima tuaangalia pia kiuchumi, lakini kwa *gap* tuliyonayo ya watumishi wa umma ni kubwa sana na wataalam tunao lakini shida ni kwamba tunawaingizaje kwenye *payroll*, *issue* hapa ni mshahara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaendelea nalo na tutakuja nalo tukuhakikishie kabisa kwamba, tunayo dhamira ya dhati na

hili likiwezekana litaondoa kabisa ombwe lililopo kati ya watu ambao wanadhurura kufanya shughuli zingine badala ya zile walizozisomea. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana. Sasa Waheshimiwa Wabunge ili nisiwasubirishe na salamu za kumpokea Mheshimiwa, ngoja tumpokee halafu tuendelee na maswali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kwanza kumkaribisha sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko tunakukaribisha sana Bungeni ukiwa na nafasi nyingine siyo kwamba wewe ni mgeni Bungeni lakini nafasi yako ndiyo inatufanya tukukaribishe tena Bungeni, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia nitumie fursa hii kwa niaba yenu na wananchi wote kwa ujumla kukupongeza sana kwa imani ambayo Mheshimiwa Rais ameionesha kwako kwa nafasi hiyo kubwa ambayo sote tunaifahamu ni ya kihistoria, kwa sababu huwa haiji mara nyingi inakuja mara chache na katika hizo chache wewe umepata hiyo nafasi. Kwa hiyo, tunakupongeza sana. *(Makofi)*

Katika majukumu yako hayo mapya tutaendelea kukupa ushirikiano kama ambavyo tumekuwa tukikupa ushirikiano na sasa unazo hizo nafasi mbili na katika hizo zote tutakupa ushirikiano usiwe na wasiwasi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu lakini pia ni Waziri wa Nishati, kwa hiyo kuna wakati pengine atatakiwa kuja kwenye hizo Kamati muwe mnakumbuka tu kwamba ana nafasi mbili, msije kuwa mnamuita ita kama vile mlivyokuwa mnamuita huko nyuma, mtazame hayo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, kwa ujumla tunakupongeza sana na tunakutakia kila la kheri katika majukumu yako, Kwa sababu sasa tunampongeza yeye lakini pia tunalipongeza Baraza zima la Mawaziri, wale ambao walikuwepo na wamesalia

tunawapongeza sana kwa kuendelea kuaminiwa, na wale wapya ambao wameungana nanyi wote kwa ujumla tunawatakiwa kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yenu na Bunge litaendelea kuwapa ushirikiano. *(Makofi)*

Wale wapya kabisa muendelee kujifunza kwa wenzenu waliotangulia na wale ambao mmepumzika kidogo msiwe na wasiwasi, hili Baraza linao Mawaziri ambao walishawahi kupumzika wakarejea, wakapumzika tena, wakarejea. Kwa hiyo, msiwe na wasiwasi hizi nafasi huwa ni kwa zamu na mtu zamu yake inapofika basi anafanya hiyo kazi, zamu yake inapopungua kidogo, ni kama kocha anaweka huyu si kwamba wewe uliyetoka ni mbaya ama namna gani, hapana! Kocha anataka akupumzishe pengine kwa ajili ya maandalizi ya shughuli nyingine hapo baadaye au kama ni timu za Simba na Yanga basi huenda timu inayokuja baadaye inaweza kuwa ni Namungo halafu ukapumzishwa kidogo ili wacheze na Namungo kwa sababu mechi inayokuja ni ngumu zaidi. Ahsanteni sana, tunawapongeza sana Baraza la Mawaziri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mbunge wa Lindi Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 60

**Ujenzi wa Soko la Samaki – Lindi Manispaa**

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga soko kubwa la Samaki Lindi Manispaa?

**SPIKA:** Samahani, najaribu kuangalia Mheshimiwa umekaa wapi? Maana sasa natazama kule nasikia sauti, simuoni Mbunge, haya ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa naomba nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kila kitu, pia ninaamshukuru sana Mheshimiwa Rais Mama yetu Samia Hassan Suluhu kwa imani yake kubwa kwa kunipa nafasi hii nimsaidie kumuwakilisha katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mbunge wa Lindi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya uvuvi nchini, ikiwemo masoko ya samaki katika Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi, kwa kuzingatia upatikanaji wa maeneo na rasilimali fedha. Changamoto iliyopo ni upatikanaji wa maeneo katika Halmashauri zetu kwa ajili ya ujenzi wa masoko. Kwa sababu hii, nimuombe Mheshimiwa Mbunge kwa nafasi yake, asaidie kupatikana kwa eneo la ujenzi wa soko hilo katika Manispaa ya Lindi na mara likipatikana, Wizara yangu itafanya tathmini za awali ikiwa ni pamoja na kuandaa michoro na gharama za ujenzi. Aidha, baada ya kukamilika kwa hatua hizo, Wizara itatafuta fedha za ujenzi wa soko hilo katika vyanzo vya ndani, yaani bajeti ya Wizara au miradi kwa ajili ya kuanza ujenzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, swali la nyongeza.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu hayo ya Serikali yenye kuleta matumaini kwa wananchi wa Lindi Manispaa. Hata hivyo, naomba sasa niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Lindi Manispaa tumeshatenga ekari moja na nusu kwa ajili ya ujenzi wa soko hili la samaki, vilevile tuna wavuvi 2,193 ambao wamesajiliwa na wachuuzi wadogo

wadogo 470 ambao wanakosa mahali pa kufanyia shughuli zao za biashara. Naomba Serikali itupe majibu ya uhakika na ya kueleweka ya kuwapa wananchi wa Lindi Manispaa matumaini; ni lini sasa mtaanza kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa soko la Samaki?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake kwa wavuvi kwa kuwakopesha maboti, pamoja na nyavu na injini ili wavuvi hawa sasa waendeleze uvuvi wao kwa vifaa hivi vyenye uhakika na usalama wa kutosha? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tujitahidi kupunguza sauti kidogo ili tuwe tunasikilizana.

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Mbunge alivyouliza swali lake la nyongeza kuwa tayari Halmashauri ya Manispaa ya Lindi tayari wameshakupata eneo, namwomba baada ya Bunge hili twende na wataalamu pale Lindi tukahakiki hilo eneo na wataalamu na tukishajua eneo hilo lililopatikana lina ukubwa gani na linafaa kwa matumizi hayo, Wizara iko tayari kuanza ujenzi wa soko hilo mara moja.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ameuliza kuhusu zana. Tathmini tayari imeshafanyika, wataalamu wameshafanya tathmini ya zana gani zinafaa kwa maeneo hayo ya wavuvi, namwomba baada ya hili, kwa sababu tayari kila kitu kimeshafanyika, basi baada ya Bunge hili tuambatane naye kama nilivyosema hapo awali, twende kwa wavuvi hao kuhakiki ni aina gani ya zana zinazohitajika ili Serikakli ione namna ya kuanza kuwakopesha wavuvi hao hizo zana, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Ni lini Serikali itaanza mpango wa kujenga soko jipya la kisasa la samaki katika Wilaya ya Kigamboni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, swali la nyongeza Mheshimiwa Ndugulile, anataka kujua ni lini Serikali itaanza ujenzi wa soko jipya Kigamboni. Ujenzi wa soko jipya Kigamboni utategemea uwezekano wa kibajeti. Kama Serikali itapata bajeti, basi iko tayati kuanza ujenzi wa soko hilo jipya pale Kigamboni, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa naona mmesimama, hamumpi nafasi kidogo ya kujifunza mambo ya Wizara? Mheshimiwa Husna Sekiboko, swali la nyongeza.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, swali dogo la nyongeza. Hali ya soko la samaki Tanga ni sawa sawa kabisa na hali ya soko la samaki Lindi; je, ni upi mkakati wa Serikali katika kuhakikisha linapatikana soko la samaki la kisasa kwenye Jiji la Tanga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kama alivyouliza Mheshimiwa Mbunge katika swali lake, wako wataalam wanafanya tathmini ya kuyatambua hayo masoko yote nchi nzima. Tunaomba nafasi ili wataalam hao waendelee na tathmini hiyo, na wakishamaliza, Serikali itatoa utaratibu wa namna gani masoko hayo yanakwenda kujengwa katika nchi yetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Miundombinu ya soko la samaki katika Manispaa ya Mtwara

Mikindani ni mibovu na mibaya hasa sehemu ya jiko pamoja na ofisi. Nini mkakati wa Serikali kuboresha miuondombinu hiyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, soko la Mikindani ni kama masoko mengine ambayo nimeshatoa maelekezo, kwamba tutatuma wataalam kuja kuangalia upungufu uko wapi, halafu baada ya kuyajua huo upungufu, Serikali iko tayari kuanza kufanya marekebisho ya maeneo hayo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 61

**Uwekaji wa samani Chuo cha *FETA* Mikindani**

**MHE. AGNES E. HOKORORO** aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kuharakisha uwekaji samani kwenye maktaba na maabara Chuo cha *FETA* Mikindani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024 Serikali kupitia Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi *(FETA)* inaendelea na uboreshaji wa miundombinu ya kufundishia katika Kampasi zake ikiwemo ujenzi wa maabara na maktaba katika kampasi ya Mikindani. Pindi tuu ujenzi wa majengo hayo ya maktaba na

maabara yatakapokamilika katika kampasi ya Mikindani, Serikali itaweka samani kwenye miundombinu hiyo muhimu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba kuuliza maswali mawili madogo nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sasa ni mwaka wa tano tangu 2018 maktaba ilipokamilika, thamani zake ziko wapi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, maabara ilipanga kukamilika Oktoba, 2022 na kwa sasa imefikia asilimia 35, nini tamko la Serikali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwamba Wizara ilikuwa inasubiri ukamilishaji wa maktaba na maabara na baada na ukamilishaji huo, Serikali inakwenda kuweka samani zote. Kwa kuwa tayari maktaba imeshakamilika, bado maabara, Wizara ilikuwa inasubiri vyote vikamilike kwa pamoja ili samani hizo zote ziende kwa pamoja. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge avute Subira, jambo hili tunalifuatilia. Leo jioni tukutane mimi na yeye twende pale Wizarani tufuatilie tuone jambo hili linafika mwisho kwa kiwango hiki, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, mbona umechagua leo jioni? Mheshimiwa John Kanyasu, swali la nyongeza. *(Makofi)*

**MHE. CONSTATININE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, nime-*withdraw* swali langu la nyongeza.

**SPIKA:** Aah, haya, ahsante sana, nilikuwa sijasikia. Unajua wakati Kiingereza mwingine kigumu sana.

Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 62

**Umuhimu wa elimu ya *Biogas* kwa wafugaji**

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatoa elimu kwa wafugaji kuhusu matumizi ya *biogas* ili kuhamasisha ufugaji wa kisasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imekuwa ikitoa elimu ya ufugaji bora ikiwa ni pamoja na matumizi ya samadi kuzalisha *biogas* ambayo ni nishati mbadala ya kupikia na rafiki kwa mazingira.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya nishati mbadala ya *biogas* ambayo inatokana na kinyesi cha mifugo ikitumika vizuri, itapunguza matumizi ya kuni na mkaa hivyo kuboresha maisha ya wafugaji na kuhifadhi mazingira. Kutokana na umuhimu huo, Wizara kupitia Wakala ya Mafunzo ya Mifugo *(LITA),* inatoa mafunzo ya utengenezaji wa *biogas* kwa wanafunzi wanaosoma katika vyuo vyake katika ngazi ya cheti na *diploma* ili watakapohitimu masomo hayo, wawe na ujuzi wa teknolojia ya *biogas* na waweze kuwafundisha wafugaji matumizi sahihi ya teknolojia hiyo pia. *LITA* hutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wafugaji au vikundi vya wafugaji vinavyohitaji mafunzo hayo katika kampasi za Mpwapwa na Tengeru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka, swali la nyongeza.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Shirika la *CARMATEC* limebobea katika kutengeneza mitambo ya *biogas;* je, Serikali inajishughulishaje na shirika hili karika mambo ya utengenezaji wa *biogas*?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kwa kuwa nchi ya China inaongoza kwa uzalishaji wa *biogas* kwa kiwango cha *cubic meters* 15,000,000 kwa mwaka; je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka wananchi wetu wakasome wapate ujuzi wa hali ya juu wa kutengeneza *biogas;* kwanza kwa sababu tunahitaji kufuga zaidi kisasa kuliko kuswaga ng'ombe; na pili itapuguza uharibifu wa mazingira kwa ajili ya mmomonyoko wa udongo unaoletwa na ng'ombe wengi ambao wanachungwa badala ya kufungwa? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Mbunge anataka kujua namna ambavyo Serikali na Wizara yetu inavyoshirikiana na mashirika haya ikiwa ni pamoja na wadau wetu wa China. Wizara imepokea ushauri huo wa Mheshimiwa Mbunge. Tutakwenda kulifanyia kazi jambo hili la mashirikiano yetu na kupeleka wanafunzi wetu kwenda kujufunza nchini China.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, jambo hili tumelichukua na ushauri huu tumeupokea na tutakwenda kulifanyia kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 63

**Uhaba wa maji Same**

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kutatua tatizo la uhaba wa maji tambarare ya Same wakati ukisubiriwa Mradi wa Maji wa Mwanga – Same hadi Korogwe?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, wakati utekelezaji wa mradi mkubwa wa Same – Mwanga – Korogwe unaendelea na unaotarajia kukamilika mwezi Juni, 2024 na kunufaisha baadhi ya maeneo ya Wilaya za Same, Mwanga na Korogwe, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kutatua changamoto ya maji kwa wananchi wa Wilaya ya Same. Mathalani katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imekamilisha miradi ya maji katika Vijiji vya Kirinjiko, Mabilioni Kijomo na Gunge na tayari inatoa huduma iliyokusudiwa kwa wananchi. Aidha, visima vitatu vimechimbwa katika eneo la Mahuu kwa ajili ya kuhudumia eneo la Same Mjini ambapo kwa jumla vina uwezo wa kuzalisha jumla ya lita 720,000 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha 2023/2024, Serikali itafanya utafiti wa maji chini ya ardhi pamoja na kuchimba visima virefu viwili katika maeneo ya Same Mjini na Kijiji cha Marondwe, Njoro ili kuongeza vyanzo zaidi vya maji. Utekelezaji wa visima hivyo unatarajiwa kuanza mwezi Januari, 2024 mara baada ya uchimbaji kukamilika na maji kupatikana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Napenda kujua kama ratiba ya kukamilisha mradi mkubwa wa maji kutoka Mwanga kwenda Same mpaka Korogwe imebaki pale pale mpaka mwaka kesho mwezi wa Nne wananchi wa Same wanapata maji kutoka Mwanga?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa sasa hivi wananchi wangu wa Same hawana maji: Serikali ina mpango gani wa dharura kuchimba visima virefu katika Kijiji cha Ishire, Kitongoji cha Kavambuhu, Majevu, Kirinjiko, Makanya pamoja na Mabilioni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza. Wizara tutafanya kila jitihada kuhakikisha mradi huu unakamilika ndani ya wakati kadiri tulivyosaini mkataba na mkandarasi.

Mheshimiwa Spika, kwa suala la dharura, maeneo yote yenye dharura kama Same Mjini na hasa maeneo haya aliyoyataja Mheshimiwa Mathayo, tutafanya kila jitihada kuona mashine ambazo Mheshimiwa Rais ametununulia tuweze kuondoa changamoto hii, basi tutakwenda kuchimba hivi visima. Lengo ni wananchi kupata huduma kwa wakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Wananchi wa Kiegea, Mkundi pamoja na Kilimanjaro bado hawapati maji ya kutosha; je, ni lini watapata maji ya kutosha kutoka kwenye mradi wa Mguu wa Ndege? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, kama ifutavyo: -

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Christine. Huu mradi mimi na yeye akiwa Mwenyekiti wa Kamati tulifika na kuufuatilia kwa karibu sana na anaendelea kuufuatilia. Mpaka sasa tumeshaweza kutekeleza mradi kwa asilimia 86. Maeneo ya Kihonda Kaskazini na Kilimanjaro, hivi navyoongea tayari wameshaanza kupata huduma.

Mheshimiwa Spika, maeneo haya aliyoyataja Mheshimiwa Dkt. Christine na yenyewe pia tunaendelea kufanya jitihada kuona kwamba kufikia Desemba, mwaka huu 2023 na yenyewe pia yaweze kupata huduma ya uhakika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Eric Shigongo, swali la nyongeza.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mji wa Nyeunge una idadi kubwa sana ya watu na unahudumiwa na mradi wa maji wa Rumea, Karebezo hadi Nyeunge ambao ulijengwa chini ya kiwango; je, Serikali iko tayari kuufanyia kazi mradi huu ili uweze kutoa huduma ya uhakika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Eric Shigongo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, suala hili la ukarabati wa mradi, Mheshimiwa Mbunge ameshafika ofisini na tumeweza kuongea pamoja na wataalam. Naomba nimhakikishie, tulivyomuahidi mradi huu ni lazima tunakwenda kuutekeleza na tutahakikisha ukarabati uwe na tija na huduma inayotarajiwa ya maji safi na salama bombani iweze kupatikana kwa wakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba kuuliza swali la nyongeza. Ni lini Serikali itapeleka fedha kwenye miradi ya Itununu, Tabweta ili iweze kukamilika na wananchi wa Tarime wapate maji safi na salama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Michael Mwita, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, miradi hii aliyoitaja ipo katika mpango wa kulipa fedha katika miezi hii ya Julai na Agosti. Fedha zimechelewa kufika, lakini kuanzia wiki hii wakandarasi wapo kwenye utaratibu wa kuweza kulipwa kwa lengo la kuendelea na utekelezaji wa miradi hii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Majala, swali la nyongeza.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Jiji la Dodoma limeendelea kukumbwa na kadhia kubwa ya uhaba wa maji: Je, Serikali ni lini mtakamilisha mradi wa visima vya Nzuguni ili kuondoa kadhia hii inayowakumba wananchi na wakazi wa Jiji la Dodoma? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kunti Majala, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ukamilishaji wa visima vya Nzuguni, kadiri tunavyopata fedha tutaendelea kumwezesha mkandarasi ili viweze kukamilika ndani ya miezi ya mkataba tuliyokubaliana naye. Tunafahamu changamoto kubwa inayokumba Jiji la

Dodoma na tunaendelea na jitihada nyingi sana kuona kwamba pamoja na visima hivi na vyanzo vingine, tuweze kuondoa adha ambayo ipo kwenye Jiji la Dodoma.

**SPIKA:** Mheshimiwa Angeline Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niruhusu nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa fursa ambayo nimeipata kuja kuuliza swali hapa. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa imani yake kubwa kwa kuniamini, nimefanya kazi na nimetua kijiti kwa Mheshimiwa Silaa na niko tayari kutoa ushirikiano wakati wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina swali la nyongeza. Kwanza natambua kwamba Serikali imeweka katika bejeti yake kuongeza chanzo kingine cha maji katika Jiji la Mwanza, hususan Manispaa ya Ilemela kutokana na changamoto kubwa ya maji katika mji ule: Je, ni lini utekelezaji wa mradi huo wa chanzo kipya cha maji utaanza kutekelezwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula Mbunge wa Ilemela kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nipende kumpongeza kwa sababu suala hili amesha lileta mara kadhaa katika ofisi zetu na niseme tu jitihada zako zimesababisha Mheshimiwa Waziri Jumaa Hamidu Aweso kukuletea Mkurugenzi wa mamlaka mpya mwanamama, mchapakazi. Jitihada zako zimesababisha kuileta *task force* ya wataalam kuona kwamba Mwanza sasa inaenda kupata suluhu.

Mheshimiwa Spika, chanzo hiki kipya Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula naomba nikupe amani kwamba kadri wataalam wetu watakapo kamilisha kazi waliyopewa na Mheshimiwa Waziri Jumaa Hamidu Aweso, chanzo hiki mara moja kinakwenda kufanyiwa kazi ndani ya mwaka huu wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, swali la nyongeza.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii. Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu imechimbiwa visima zaidi ya kumi na tano lakini hadi sasa havijapata *pump* ya kuendesha visima hivyo. Je, ni lini Serikali itatoa fedha ili visima vyote ambavyo vimechimbwa ndani ya jimbo langu viweze kufanya kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Yahya Ally Mhata kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, visima vilivyoko Nanyumbu tunavishughulikia na manunuzi ya *pump* yako kwenye hatua za mwisho.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, Mbunge wa Sumve sasa aulize swali lake.

Na. 64

**Tatizo la mawasiliano ya simu Sumve**

**MHE. KASALALI E. MAGENI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itahakikisha tatizo la kutokuwepo mawasiliano ya simu ya uhakika katika maeneo mengi ya Jimbo la Sumve linatatuliwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kasasali Emmanuel Mageni, Mbunge wa Jimbo la Sumve kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* imefikisha huduma za mawasiliano katika Kata za Bugando, Lyoma, Mwandu, Ngulla na Sumve.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali itafanya tathmini katika Jimbo la Sumve ili kubaini maeneo ambayo bado yana changamoto za upatikanaji wa huduma za mawasiliano ili yatafutiwe fedha kwa ajili ya kutatua changamoto hizo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kasalali Mageni, swali la nyongeza.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, kwanza ili kuweka kumbukumbu sawa naomba nirekebishe jina langu kama lilivyotajwa na Mheshimiwa Waziri, mimi ninaitwa Mheshimiwa Kasalali na sio Kasasali.

Mheshimiwa Spika, baada ya marekebisho hayo, naomba niishukuru Serikali kwa majibu mazuri na nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa utayari wake alipokuja kwenye Jimbo la Sumve kusikiliza changamoto zetu.

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza, kwa kuwa kumeibuka aina mpya ya kangomba katika sekta ya mawasiliano ambapo kampuni za simu mara baada ya kufanya utafiti wa maeneo ambayo wataweka minara wamekuwa wakishirikiana na wajanja wachache wanaokwenda kuyatwaa maeneo haya kwa kuwalaghai wamiliki na hatimaye wao kuingia kwenye orodha ya watu wanaopangishwa na minara hiyo ya simu.

Je, nini tamko la Serikali juu ya ulaghai huu ambao umekuwa ukifanywa kupitia makampuni ya simu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ...

**SPIKA:** Mheshimiwa kwa kifupi.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kata za Wala, Mwabomba na Maligisu hali ya mawasiliano ni mbaya sana na Serikali imesema inao mpango wa kupeleka mawasiliano katika maeneo hayo. Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kupeleka mawasiliano haraka sana katika kata hizo ili kurahisisha mawasiliano kwa watu hawa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuomba radhi kwa kukosea jina la Mheshimiwa Mbunge. Napenda sasa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni Mbunge wa Sumve kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kama ambavyo nimejibu katika majibu yangu ya msingi, kuna maeneo ndani ya jimbo hili bado kuna changamoto na ndio maana Serikali tunaenda kufanya tathmini ili tujiridhishe ni hatua gani ambazo tunazichukua aidha kama ni kujenga mnara au kuongeza nguvu. Lengo ni kwamba mawasiliano ndani ya Jimbo hilo la Sumve yaweze kuimarishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa swali la ulaghai. Nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge, lakini kwa picha ambayo nimeiona nikiwa nafanya ziara. Kumekuwa na maeneo ambayo yamekuwa na changamoto kweli, watoa huduma kuhusishwa na jambo kama hili.

Mheshimiwa Spika, lazima nikiri kwamba sina uhakika na uthibitisho wa namna ambavyo watoa huduma wanashiriki, isipokuwa naamini kwamba kuna wajanja ambao wanahisi

kwamba eneo fulani linakwenda kujengwa mnara basi wao wanawahi kwenda kulinunua ili baadaye wao ndio waweze kulipwa.

Mheshimiwa Spika, pia ninaamini kwamba kwa kushirikiana na Ofisi ya Halmashauri kwa sababu tulishatoa maelekezo, ujenzi wa minara ni lazima Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ihusishwe katika hatua zote ili kuhakikisha kwamba tumeondokana na migogoro ambayo inaweza ikatokea kwa sababu ya ujenzi wa minara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia fursa hii. Nina swali la nyongeza. Jimbo la Newala vijijini maeneo yake mengi yanakosa mawasiliano ya simu. Je, ni lini Serikali itakuja kujenga minara katika jimbo lile ili mawasiliano yaweze kuboreshwa? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri, mimi pamoja na Mheshimiwa Mbunge tumeshafanya ziara katika jimbo lake na maeneo ambayo yalikuwa na changamoto, Serikali iliyachukua na tayari yameingizwa kwenye utekelezaji wa miradi 758 ambapo kata 713 zinaenda kuguswa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi bali awe na subira wakati utekelezaji ukiwa unaanza, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Kata za Masanga na Ngofia katika Jimbo la Kishapu hazina mawasiliano kabisa ya simu. Je, ni lini Serikali itapeleka minara katika kata hizo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kati ya majimbo ambayo yamepata minara mingi sana, minara zaidi ya tisa ni katika Jimbo la Kishapu na utekelezaji wake uko katika hatua mbalimbali na umeshaanza. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge aendelee kushirikiana na watoa huduma ili miradi hii ikamilike kwa wakati, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, swali la nyongeza.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itatatua tatizo la mawasiliano katika Kata ya Mchuki pamoja na Mbuchi kwenye Jimbo la Kibiti?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, Mbunge wa Kibiti kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Kibiti kuna maeneo ambayo yana changamoto ya mawasiliano. Vilevile kuna maeneo ambayo tayari Serikali imeyaingiza katika ile miradi 758. Kama kuna maeneo ambayo yatabaki kuwa na changamoto Serikali inayapokea ili iwatume wataalam wake wakafanye

tathmini na tujiridhishe ukubwa wa matatizo yaliyopo pale *then* tupate fursa ya kupeleka huduma ya mawasiliano, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nashoni Bidyanguze, swali la nyongeza.

**MHE. NASHONI W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza Serikali. Ni lini itapeleka mawasiliano katika Kijiji cha Songambele, Kalilani, Mkanga pamoja na Chagu? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge wote. Miradi ya Mawasiliano ambayo tumesaini mwezi wa tano iko katika hatua za awali za utekelezaji wake. Ninaamini kabisa kwamba kwa sababu Waheshimiwa Wabunge hawajaanza kuona minara ikiwa ina simama katika maeneo yao, wavute subira ili tutakapoanza utekelezaji wake na baadaye minara itakapoanza kuonekana basi tutaweza kubaini maeneo ambayo yatakuwa bado yanahitaji kupelekewa mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Songambele, tayari imeingizwa katika vijiji 2116 ambavyo vinafanyiwa tathmini na tayari Serikali imeshaanza kutafuta fedha ambapo Mheshimiwa Rais alishapata fedha ya kufikisha minara 600 mingine. Ninaamini Mheshimiwa Mbunge, atakuwa mmoja wa wanufaika katika minara hiyo 600, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, swali la nyongeza.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kumekuwa na changamoto kubwa sana ya mawasiliano katika Kata ya Makanya, Mbwei na Maibwi; je, ni lini Serikali itapeleka mawasiliano katika Kata hizo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, tayari tulishawasiliana na Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi na amekuwa akinijulisha kuhusu changamoto hiyo. Maeneo na kata ambazo zina changamoto hizo tayari Serikali imeshazipokea na imeziingiza kwenye mpango wa utekelezaji wa miradi ambayo inakuja kadri ya upatikanaji wa fedha utakavyoruhusu, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Ipande Kijiji cha Mhanga, Kata ya Sanjalanda Kijiji cha Gurungu, Kata ya Mgandu Kijiji cha Itagata na Kata ya Wamagande Kijiji cha Kitanura hakuna mawasiliano kabisa. Nini kauli ya Serikali kuwapelekea wananchi hawa minara ya mawasiliano ya simu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Omary Massare kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Tanzania ya sasa ni Tanzania ya Kidigitali, hatutahitaji mtanzania yeyote aachwe nyuma, kwa hiyo naomba nipokee changamoto hizi ili tupeleke wataalam wakaangalie ukubwa wa tatizo ili tupeleke huduma ya mawasiliano na watanzania wote washiriki katika uchumi wa kidigitali, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba George, swali la nyongeza.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Serikali iliahidi kujenga minara ya mawasiliano kwenye Kata

ya Bugarama na Kata ya Kibogora lakini kazi haijaanza hadi sasa. Ni lini Serikali itakuja Ngara kwenye Kata hizo kujenga minara ya mawasiliano? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro Mbunge wa Ngara kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mwenyewe na Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro tulishatembelea jimbo lake na tulizunguka katika maeneo yote ambayo yana changamoto ya mawasiliano na baada ya kugundua changamoto hiyo Serikali ikaingiza katika mpango wa utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, katika mpango huo wa utekelezaji, tayari watoa huduma wameshapatikana lakini utoaji wa huduma hii una mchakato kidogo unaposaini, lakini kuna masuala ya vibali kwenda kupata ardhi kuingia mikataba na wenye ardhi, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba maeneo haya kwa kuwa Serikali imeshaahidi hakuna eneo ambalo litaachwa bila kujengwa mnara, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Maliasili na Utali, Mheshimiwa Yustina Aracadius Rahhi, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake,

Na. 65

**Kuanzisha Mfuko wa Fidia kwa wahanga wa wanyamapori**

**MHE. YUSTINA A. RAHHI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanzisha Mfuko wa Fidia kwa wahanga wanaoathirika na wanyamapori wakali na waharibifu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la kama ulivyonielekeza.

Mheshimiwa Spika, kwa hii ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako tukufu baada ya Mheshimiwa Rais kunipa heshima hii ya kuniteua kuwa Naibu Waziri, naomba nitumie fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye imempendeza niweze kutumika kwenye nafasi hii.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pili nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kunipa heshima hii ya kuitumikia nchi yetu. Naahidi kutekeleza majukumu yangu kwa uwezo wangu wote na kwa vipawa vyote alivyonipa Mwenyezi Mungu, naahidi sitamwangusha.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba ushirikiano wako na Wabunge wenzangu nawaahidi ushirikiano naomba tushirikiane.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikilipa kifuta jasho na kifuta machozi kama mkono wa pole au faraja kwa wananchi wanaopata madhara kutokana na wanyamapori wakali na waharibifu. Malipo hayo yamekuwa yakifanyika kwa mujibu wa Kanuni za Kifuta Jasho na Machozi za mwaka 2011 na kwa kadri ya upatikanaji wa fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, kanuni hizo zilianza kutekelezwa mwaka 2012 ambapo katika kipindi cha kuanzia 2012/2013 hadi 2022/2023 jumla ya shilingi bilioni 11.3 zimelipwa kwa wananchi walioathiriwa na wanyamapori wakali na waharibifu. Hata hivyo, suala hili limekuwa ni changamoto kubwa kwa nchi nyingi za Afrika ambapo limesababisha baadhi ya nchi kuondokana na utaratibu wa kulipa kifuta jasho na machozi. Lakini Tanzania imeendelea kuona umuhimu wa kuwafuta jasho na machozi

wananchi kwa madhara wanayoyapata kutokana na wanyamapori hao.*( Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Yustina Rahhi, swali la nyongeza.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, ninaishukuru Serikali kwa majibu mazuri. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitoa kifuta jasho kwa wahanga walioathirika na wanyamapori ikiwepo laki moja tu kwa heka nzima ya mazao yaliyoharibiwa au shilingi laki mbili kwa mtu aliyejeruhiwa, laki tano kwa aliyepata jeraha la kudumu na labda milioni moja kwa familia ya aliyeuawa na wanyama pori na pengine kuchelewesha kutoa malipo hayo kwa wahanga.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu matukio hayo yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku pengine kuwa mzigo mkubwa kwa Serikali na kushindwa kuwalipa kama ilivyo nchi ya jirani ni kwa nini sasa Serikali isione umuhimu wa kuanzisha huu mfuko wa fidia kwa wahanga?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kwa kuwa Serikali yetu ya Tanzania bado inatoa kifuta jasho kwa wahanga, haioni sasa ni muda mwafaka kurejea na kubadilisha baadhi ya mafungu katika Sheria hiyo ya Wanyamapori ya mwaka 2011 hasa kuongeza nyongeza hii ya fidia angalau iendane na hali ya maisha ya sasa? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu**.**

**NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli imekuwepo changamoto ya viwango vya fidia au kifuta jasho kuwa vidogo. Vilevile ni kweli kwamba wakati mwingine imechukua muda mrefu kwa wananchi hao kufidiwa. Serikali imeliona hili na imelifanyia kazi na

tuko kwenye hatua za mwisho za kuona kwamba kanuni zinafanyiwa marekebisho ili wananchi waweze kulipwa stahiki zao kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na hili la kusema tuanzishe mfuko maalum. Serikali imefanyia kazi jambo hili na imefanya utafiti kwa nchi jirani ambazo zimekuwa na mfumo huu na imejiridhisha kwamba wenzetu wamepata matatizo kuendana na mfumo huu unaopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali inajielekeza kuweka mikakati ya dharula ambayo itatuhakikishia kwamba tunaondokana na tatizo hili, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, swali la nyongeza.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata nafasi. Wako wananchi wangu wa Kata ya Maore, Karemawe, Bendera nakadhalika ambao wameuawa na Tembo takribani miaka miwili sasa lakini Serikali haijatoa kifutajasho wala chochote.

Je, hauoni kwamba Serikali inaonekana kama inawathamini Tembo zaidi kuliko ambavyo inawaona wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukulia kwa umuhimu na uzito mkubwa maisha ya Watanzania. Kutokana na changamoto hizi ambazo zimekuwa zikijitokeza kwa tembo kuvamia na kupoteza maisha ya wananchi wetu, Serikali imeandaa mkakati wa dharura ambao utatuondoa kwenye changamoto hii. Naomba tuipe Serikali muda, ndani ya kipindi mfupi tutaona matokeo ya utekelezaji wa jambo hili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Mariam Kisangi.

Na. 66

**Kudhibiti popo eneo la Upanga – Dar es Salaam**

**MHE. MARIAM N. KISANGI K.n.y. MHE. NEEMA W. MGAYA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaondoa popo waliopo maeneo ya Upanga ili kulinda afya za wakazi wa maeneo hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kudhibiti popo katika Jiji la Dar es Salaam kwa kuchukua hatua mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kufanya soroveya *(survey)* ya kuangalia ukubwa wa tatizo, maeneo yaliyoathirika, mbinu gani ambazo ni rafiki kwa mazingira zitumike kudhibiti na pia kubaini aina ya popo wanaosumbua. Imebainika kuwa kuna aina mbili ya popo wanaosumbua, ambao ni popo wanaokula matunda (hawa wanaotumia miti kama maeneo yao ya makazi) na popo wanaotumia mapango au magofu ya nyumba kama makazi yao.

Mheshimiwa Spika, katika kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo, majaribio ya dawa tano za kunyunyizia yalifanyika ili kufukuza popo katika makazi hayo. Kati ya dawa hizo; dawa mbili *(Napthalene* na *Bat CRP)* zimeonekana kuwa na uwezo wa kuwafukuza popo hao. Juhudi zaidi zinaendelea kwa kushirikiana na wadau kwenye maeneo husika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nampongeza sana; lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imeonesha wazi kwamba wameweka hiyo dawa. Hata hivyo, tatizo la popo katika maeneo ya Upanga, *Sea View, Leaders Club*, Kinondoni, Oysterbay, Masaki, Msasani Peninsula na maeneo mengine ya ukanda wa pwani linaongezeka siku hadi siku na kusababisha popo hao mpaka wanavunja vioo vya madirisha kwenye nyumbani.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza hiyo dawa ili popo hawa waweze kuondoka na kuwaondolea adha wananchi wa maeneo hayo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa changamoto inayowapata wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam katika maeneo ya Upanga na mengineyo, pia inawakuta wananchi wa Dodoma kuvamiwa na nyuki katika maeneo mbalimbali hasa maeneo ya *Area D* katika majengo ya *TBA*, Makole yote pamoja na maeneo mbalimbali ya Jiji la Dodoma nyuki wanavamia na kuhama hama hovyo hovyo;

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaondolea wananchi wa Jiji la Dodoma adha ya kuvamiwa na nyuki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye swali la msingi, hatua ya kwanza ya kukabiliana na popo hawa ilikuwa ni kufanya

utafiti wa kujua kiwango cha ukubwa wa tatizo na aina ya dawa ambayo inaweza kutumika ili kukabiliana na changamoto hii.

Mheshimiwa Spika, utafiti huu umekamilika, sasa jukumu lililopo mbele yetu ni kuhakikisha kwamba wadau wote wanaohusika na kukabiliana na jambo hili, zikiwepo Halmashauri zetu zinachukuwa hatua ya kuhakikisha tunasambaza dawa hizi kwa wananchi ili tuweze kukabiliananа tatizo hili. Niombe wadau wote wanaohusika tushirikiane ili tuweze kuondokana na tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili la tatizo la uvamizi wa nyuki kwenye Mkoa wa Dodoma. Nitumie fursa hii kuwaagiza wataalamu wetu wa idara ya nyuki kushirikiana na wenzetu wa jiji la Dodoma ili kufanya tathmini ya haraka na kuona ukubwa wa tatizo hili na kuchukua hatua za haraka za kuangamiza nyuki hawa, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri na kumpongeza, tunafanya kazi vizuri kwa pamoja na nimpongeza kwa majibu mazuri sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuongezea majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa upande wa popo, tayari tumeagiza dawa nyingine za majaribio ikiwemo *Pepzol* na *Super Dichlorvos* ambazo zinapatikana Marekani na Kenya. Imeonekana kwamba dawa hizo zikitumika ndani ya miezi miwili mpaka mitatu popo hao wanaweza wakatoweka.

Mheshimiwa Spika, pia nitoe rai kwa Halmashauri zetu za Jiji la Dar es Salaam na Halmashauri nyinginezo katika maeneo ya miti ya barabarani waweze kununua dawa hizo ili waweze kupiga kwa ajili ya kuweza kufukuza na kudhibiti popo hao.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa Jiji la Dodoma kuhusu suala la nyuki, kama ambavyo Naibu Waziri ameeleza, nako pia tutoe rai kwa Halmashauri ya jiji Dodoma nao watenge fedha ili waweze

kununua dawa hizo ili pale tutakapokuwa tumepata tathmini ya kuweza kujua ni dawa gani zinaweza kufanya kazi vizuri katika kudhibiti basi waweze kununua dawa hizo na kuweza kutumia.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia taasisi ya *TAWIRI* tutaendelea kushirikiana na wananchi pamoja na taasisi katika kuhakikisha kwamba tunadhibiti tatizo hili. Tuombe ushirikiano kwa wale wenye makazi pia waweze kununua dawa hizi katika maduka mbalimbali yanayozalisha dawa hizi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Felista Njau swali la nyongeza.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na popo katika Mkoa wa Dar es Salaam, kuna tatizo kubwa la kunguru ambao wamekuwa wakitapakaa kila mahali, wanajerui watoto; na hasa katika fukwe, ambako wamekithiri, na hivyo kuharibu utalii wetu. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha wanadhibiti kunguru hao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba kujibu swali la nyongezala la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli tumekuwa na tatizo la kunguru katika maeneo mbalimbali nchini. Serikali kupitia Wizara imekuwa ikifanya jitihada ya kuja na mipango mbalimbali ya kuweza kuondokana na tatizo hili. Changamoto tunayoiona ni kwamba wenzetu kwenye maeneo ya halmashauri zetu wameliacha jambo hili kuwa ni jambo la Wizara peke yake. Tunawaomba sana wadau wenzetu katika maeneo ya halmashauri, kwa kutumia teknolojia iliyoandaliwa na Wizara tushirikiane ili kupambana na tatizo hilo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea, Naibu Waziri ni wa Maliasili na Utalii; sasa nikawa nawaza, juhudi hizi zote ni za kuua popo, nyuki na kunguru. Sasa tukishawaua wote tutabaki na nini? Nadhani utafutwe utaratibu mzuri, kama ambavyo tembo wakija tunawatafutia namna ya kwenda. Utafiti ufanyike ili kuweza kuwazuia wasije. lakini, tukisema tutaua wale popo wote, nyuki wote, asali itatoka wapi? Kwa sababu mwishoni tutapata changamoto. Kwa sababu, Kunguru nao wana umuhimu wao kama viumbe. Nadhani tutafute namna bora ya kuwafanya wasilete hayo madhara.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa Ali Vuai Khamis, Mbunge wa Mkwajuni sasa aulize swali lake.

Na. 67

**Kujenga Kituo cha Polisi Matemwe – Unguja**

**MHE. ALI VUAI KHAMIS** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kituo cha Polisi Matemwe Mkoa wa Kaskazini Unguja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ali Vuai Khamis, Mbunge wa Mkwajuni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Matemwe lenye Shehia sita hakuna sehemu iliyotengwa kwa ajili ya kujenga Kituo cha Polisi. Hivyo napenda kutumia fursa hii kumshauri Mheshimiwa Mbunge, aishirikishe Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini A ili itenge eneo kwa ajili ya kujenga Kituo cha Polisi pamoja na nyumba za makazi ya askari katika eneo la Matemwe ili Serikali

kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi itenge fedha kwenye bajeti kwa ajili ya ujenzi huo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ali Vuai Khamis, swali la nyongeza.

**MHE. ALI VUAI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa maeneo hayo yaliyotajwa ni maeneo ya utalii na kumekuwa na matukio ya uhalifu; je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha ulinzi wa dharura ili kuwe na amani?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa ujenzi wa nyumba na kituo cha polisi ni jukumu la Wizara; je, Serikali haioni haja ya kwenda kukaa na Serikali ya Mkoa, halmashauri na jimbo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu umuhimu wa kuimarisha usalama kwenye eneo hili lenye watalii wengi, nitumie nafasi hii kumwekeleza *IGP* na hususani Kamishina wa Polisi Zanzibar kuimarisha huduma za doria ya magari ya askari wanaokwenda kwa miguu au pikipiki ili kuhakikisha wananchi na watalii wanaotembelea eneo hilo wanakuwa salama.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la kuimarisha ujenzi wa nyumba kupitia mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (Halmashauri), hicho ndicho kipaumbele cha Wizara kwamba katika vituo vinavyojengwa hasa vile vidogo vya Daraja C ni jukumu la mamlaka zetu za Serikali za Mitaa ambazo ni moja ya kazi za msingi ya Serikali za Mitaa. Wizara imekuwa ikisaidiana na halmashauri hizi kukamilisha majengo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuendelee kushirikiana kuzihamasihsa halmashauri hizi ili watimize huo wajibu wao nasi

tutimize wajibu wa kujenga vituo vikubwa na ku–*support* vituo vidogo wanapokuwa wamefikia kiwango cha umaliziaji, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, nataka kujua Serikali ina mpango gani wa dharura wa kuhakikisha kwamba inajenga vituo vya polisi vyenye hadhi ya kipolisi kwa Wilaya ya Tarime, Sirali, Nyamwaga na Utegi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli na Mheshimiwa Mbunge anatambua kwamba Mkoa wa Tarime – Rorya ni mkoa wa kipolisi, lakini kiutawala wako chini ya Mkuu wa Mkoa mmoja. Hata hivyo, tumeanza kutekeleza mpango wa ujenzi wa maeneo haya mapya. Ninatambua kwamba Jengo la *RPC* Tarime – Rorya *almost* limekamilika na sasa, tunakwenda kwenye ngazi ya Wilaya ili kujenga vituo vya ngazi ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa mujibu wa mpango wetu vituo vya Wilaya kwenye Wilaya mpya za kipolisi viko mbioni kwa mujibu wa utekelezaji wa mpango wetu wa miaka kumi. Nyamwaga na Sirali ni sehemu ya vituo vitakavyojengwa, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, wananchi wa Kata ya Bashnet tayari wametenga eneo kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha polisi; je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho cha polisi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kituo hiki kidogo cha Polisi cha Kata ya Bashnet ni kituo cha ngazi ya Daraja C. Nimuombe Mheshimiwa Mbunge kupitia juhudi alizozifanya kama tulivyofungua kituo kipya hivi karibuni, alifanya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, waanze ujenzi kwenye eneo lao la Bashnet *then* Wizara kupitia Jeshi la Polisi itakamilisha mtakapokuwa mmefikia *stage* ya umaliziaji hasa lenta na uwekaji wa samani, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kwezi, swali la nyongeza.

**MHE. ALOYCE A. KWEZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kupata ufafanuzi. Wilaya ya Kaliua hatuna ofisi ya *OCD* (jengo la polisi la Wilaya); je, Serikali iko tayari kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi ambapo pale Kaliua eneo lipo tayari?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, Serikali ipo tayari kushirikiana na Wilaya ya Kaliua ili kuhakikisha kituo hicho kinajengwa. Kwa kuwa tayari wana eneo, tutawasiliana na *IGP* ili kwenye mpango wake wa miaka kumi wa kujenga vituo vya polisi ngazi ya Wilaya, Kaliua iweze kupewa kipaumbele pia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, swali la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuishukuru Serikali kwa kutujengea Kituo cha Polisi Kata ya Songambele; je, ni lini Mheshimiwa Naibu Waziri tutakwenda pamoja Urambo ili ukatatue migogoro kati ya wananchi na Magereza ya Urambo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** MMheshimiwa Spika, nimuombe mama yangu Mheshimiwa Margaret Sitta na nimuahidi kwamba wakati wowote nitakuwa tayari kuambatana naye. Tutaangalia ratiba yetu baada ya Bunge hili ili kwenda kuangalia tatizo lililopo kati ya wanachi na Gereza ili kupata suluhisho la kudumu, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, Mbunge wa Mvomero, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Boniphace Butondo.

Na 68

**Ujenzi wa Kituo cha Polisi Turiani – Mvomero**

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO K.n.y. MHE. JONAS V. ZEELAND** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza ujenzi wa Kituo cha Polisi Turiani kilichojengwa kwa nguvu za wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, Mbunge wa Mvomero kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa kupitia michango mbalimbali ya wananchi inayofikia shilingi milioni 36, Kituo cha Polisi Turiani kimefikia hatua ya lenta. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imepanga kutumia fedha toka Mfuko wa Tuzo na Tozo ili kuendeleza ujenzi wa kituo hicho ambacho hadi kukamilika kitakuwa kimegharimu shilingi milioni 110, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na tunakupongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo na tunatarajia kwamba wana Mvomero watapata huduma hiyo mara moja baada ya ushirikiano kutoka Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza; swali la kwanza, je, ni lini sasa mradi huu utaanza kupewa *support* na Serikali ili kuonesha jitihada za wananchi wa Mvomero walizozianzisha?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, nakumbuka mwezi Julai Mheshimiwa Naibu Waziri ulitembelea katika Jimbo la Kishapu na Wilaya ya Kishapu, ukaona jitihada za ujenzi wa Ofisi ya *OCD* pale Kishapu; na jumla ya shilingi milioni 275 zinahitajika kwa ajili ya kukamilisha mradi huo; na uliahidi utapeleka fedha hizo kuhakikisha kwamba mradi huo unakamilika;

Je, ni lini fedha hizi zitafika ili ukamilishaji wa mradi huo wa Ofisi ya *OCD* uweze kukamilika? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu hili la mradi wa ujenzi wa kituo kule Mvomero, ni ahadi yetu kwamba katika mwaka wa fedha 2024/2025 kituo hiki kimeingizwa kwenye mpango na fedha zinazopungua zaidi ya shilingi milioni 60 zitatolewa na Jeshi la Polisi ili mradi huo utekelezwe na kukamilika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kishapu, kwanza nawapongeza wananchi waliojitolea pamoja na Halmashauri yao na Mheshimiwa Mbunge kujenga kituo bora kabisa, kinachohitaji ni umaliziaji. Tumeahidi, katika bajeti ya mwaka huu zimetengwa shilingi milioni 275 kwa ajili ya ukamilishaji huo.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge hili nimhimize *IGP* kuhakikisha kwamba anapeleka fedha hizi mapema iwezekanavyo ili ukamilishaji ule ufanyike na hatimaye huduma za kipolisi ngazi ya Wilaya ziweze kutolewa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Afya, Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki sasa aulize swali lake.

Na. 69

**Kuanzisha Mamlaka ya Kupambana na Magonjwa Yasiyoambukiza**

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanzisha Mamlaka ya Kuratibu na Kupambana na Magonjwa Yasiyoambukiza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Afya imekwishaunda programu maalum ya kuzuia na kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza ndani ya Idara ya Tiba ambayo ina jukumu la kuandaa miongozo na mikakati ya kisekta kwenye mapambano dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu imekwishatekeleza jukumu hili kwa kukiongezea jukumu Kitengo cha Afya Moja *(One Health)* kusimamia magonjwa yasiyoambukiza chini ya Kurugenzi ya Menejimenti ya Maafa, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; kwa kuwa tafiti zinaonyesha magonjwa yasiyoambukizwa yanakua kila siku; je, Serikali haioni haja sasa ya kuanzisha mchakato wa kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Magonjwa Yasiyoambukizwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni tuna Hospitali ya Kilimatinde inayoendeshwa kwa ubia kati ya Serikali na Kanisa la Anglikana, lakini hospitali hii haifanyi vizuri; je, nini mkakati wa Serikali wa kuiboresha hospitali hii iweze kusaidia katika kupambana na magonjwa yasiyoambukiza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza la kwamba magonjwa haya ya kuambukizwa yanaongezeka, ni kweli yanaongeza na hasa Kusini mwa Afrika yanaongezeka sana. Sasa hata ukiangalia leo kwenye UKIMWI, wewe ni shahidi tunatoka kwenye suala la kuuangalia UKIMWI peke yake kama UKIMWI, lakini tunaangalia magonjwa kwa ujumla na *data* zinaonyesha kwamba unapomchukua mgonjwa wa matatizo ya UKIMWI ukaangalia suala la *pressure* wakati huohuo sukari na ukatibu yote kwa pamoja, matokeo yanakuwa mazuri kuliko unapotibu ugonjwa mmoja na kumwangalia kama ugonjwa mmoja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nafikiri pamoja pia na kuanzisha Taasisi kama alivyoshauri Mheshimiwa Mbunge ambayo itashughulikia hilo moja, tunaweza tukatumia fedha nyingi ambazo bora tu hizo fedha tungepeleka kuenga vituo vya afya kule kwenye jimbo lako.

Kwa hiyo, nafikiri Mheshimiwa Mbunge aendelee kukubaliana na Serikali kwa namna hii ambayo itatumia rasilimali

vizuri, lakini wakati huo huo mgonjwa huyo akaangaliwa kwa ujumla wake, kwa sababu mgonjwa anapokuja huwezi tu kusema ni mgonjwa wa *pressure* au mgonjwa sukari unamwangalia kwa ujumla wake kuanzia saikolojia na mambo mengine ambayo yanafuatana na hilo. Kwa hiyo tukiyaangalia kwa pamoja namna hiyo tutapata matokeo mazuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili la hospitali hiyo ambayo Serikali iko pamoja na Kanisa. Mheshimiwa Mbunge mwenyewe ni shahidi kwenye hii hospitali kwamba Serikali imepeleka watumishi, lakini vilevile Serikali inatoa dawa, pia wanapewa ile asilimia ya *basket fund* kwa maana ya kuboresha mambo yao. Sasa ninachofikiri kama Serikali imefanya yote hayo na bado Mheshimiwa Mbunge kama mwakilishi wa wananchi bado wananchi wake wanalalamika kwamba huduma inayotolewa bado ni ya chini maana yake inawezekana kuna suala sasa la kiutawala.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge, Manyoni Mashariki ni karibu hapa, saa nne zinatutosha mimi na yeye twende *site,* tukae kwa saa nne tuangalie mambo mengi ili tuweze kuhukumu kwa haki na kutoa maamuzi ya kuboresha hiyo hospitali kwa namna ambayo tutakuwa tuko *site*, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rose Tweve, swali la nyongeza.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa kuwa Serikali ina mapango wa kitaifa wa kupambana na haya magonjwa yasiyoambukizwa; je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha sasa tunashuka chini sasa kwenye ngazi ya Kata na Vijiji ambako kuna uhitaji mkubwa ili hawa wananchi waweze kufikiwa na huduma hizo? Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, moja ya mkakati ni kuwa Serikali inaendelea kutoa hamasa kuhusu magonjwa haya na mmekuwa mkiona kwenye *tv* zetu. Pia kama ambavyo tumesema hapa Wizara ya Afya inatengeneza miongozo na

mojawapo ya miongozo kwenye eneo la dawa, kwenye eneo la kutoa elimu na eneo la tiba. Kwa hiyo, tutaanza kushuka mpaka *level* ya zahanati na kwa mwaka huu tunaenda kusajili hawa watu wa afya jamii ambao watafanya hiyo kazi kwenye kufika kwenye vitongoji vyetu. Kwa hiyo ni wazo zuri na tunakwenda kutekeleza kwa nmna hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rorya, sasa aulize swali lake

Na. 70

**Fidia kwa wananchi wa Rorya waliopisha eneo la kupitisha umeme mkubwa**

**MHE. JAFARI W. CHEGE** aliuliza:-

Je, lini *TANESCO* watalipa fidia kwa wananchi wa Rorya waliopisha eneo la kupitisha umeme mkubwa toka mwaka 2011?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, majibu. *(Makofi/Vigelegele)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge ahsanteni sana na kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa mbele, naomba nitumie dakika moja kwa ajili ya shukrani. Kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa ajili ya rehema na baraka. Kipekee na kwa unyenyekevu mkubwa naomba kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa imani kubwa aliyoiweka juu yangu na kuniteua niweze kumsaidia kama Naibu Waziri wa Nishati nikimsaidia Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko ambaye pia ni Naibu Waziri Mkuu. Napenda nimwahidi Mheshimiwa Rais imani

hiyo aliyonijalia nitaitumikia kwa weledi na ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rorya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika*, TANESCO* tayari imekamilisha uthamini na uhakiki wa marudio ya mali zilizoathiriwa na mradi na kwa sasa ipo katika hatua za maandalizi ya malipo. Malipo hayo yanatarajiwa kuanza mwezi Novemba, 2023 na kukamilika mwezi Desemba, 2023.

Mheshimiwa Spika, tunawaomba wananchi wanaosubiri kulipwa fidia wawe na subira wakati maandalizi ya malipo yakiwa yanaendelea kufanyika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Pia nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri yenye matumaini kwa wananchi wangu wa Rorya, lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kwa kuwa Sheria ya Uthamini inatamka wazi kwamba thamani ya ardhi inapaswa kulipwa ndani ya miezi sita, lakini wananchi hawa wamedai malipo yao toka mwaka 2011 na hawajalipwa. Nataka nipate *commitment* ya Serikali itakapofika Novemba kama wananchi hawa hawajalipwa uthamini wa ardhi yao, je, Serikali itakuwa tayari sasa kurudia uthamini kwa mujibu wa Sheria inavyotamka kwamba wananchi wale walipwe ardhi kwa mujibu wa Sheria inavyotamka?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; kwa kuwa jambo hili limekuwa ni la muda mrefu toka mwaka 2011 na sasa liko ndani ya Ofisi ya Mkurugenzi nataka nipate *commitment* ya Serikali hasa Ofisi ya Wizara ya TAMISEMI, je, ni lini watalipa fedha ili wathamini

warudi *site* wakamilishe uthamini na upande wa *TANESCO* waweze kulipa fidia kwa wananchi hawa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jafari Chege, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu kurudia zoezi ikifika Novemba, zoezi hili limeshachukua muda mrefu nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali imeshatenga fedha kiasi cha milioni 350 ili wananchi 231 wanaodai fidia walipwe ikifikia Novemba, 2023. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba zoezi hili tunaenda kulikamilisha na kwa sababu limechukua muda tutafuatilia kwa ukaribu kuhakikisha kwamba linakamilika.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali lake la pili kuhusiana na kutoa fedha, tayari Serikali kupitia *TANESCO* imeshatoa fedha kiasi cha shilingi milioni 15 kwa ajili ya kukamilisha zoezi la uthamini. Tutafuatilia kuhakikisha kwamba Halmashauri ya Rorya inakamilisha taratibu hizi kwa wakati ili zoezi hili liweze kukamilika kwa wakati kwa kadri ambavyo imepangwa, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI nimeambiwa ulikuwa umesimama.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii tena kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Rorya kuhakikisha kwamba fedha hizi ambazo wenzetu wa *TANESCO* wameshazipeleka kwenye halmashauri ile ziweze kutumika mara moja na kulipa fida hiyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ezra Chiwelesa, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mradi wa Geita -

Nyakanazi na Nyakanazi - Rusumo kuna baadhi ya wananchi wa Biharamulo ambao wanapitiwa na mradi ule katika Kata nne za Rusahunga, Kaninha na Nyakahula nao pia bado hawajalipwa pesa zao za fidia. Je, ni lini Serikali itaweza kukamilisha malipo hayo kwa baadhi ya watu ambao walikuwa hajalipwa pesa zao? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nijibu maswali ya Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na fidia ya Geita - Nyakanazi tayari Serikali ilishatenga fedha bilioni sita na tayari fedha bilioni 5.9 zilishalipwa kwa ajili ya wananchi na wananchi waliobakia ni wananchi 49 tu, tunaamini taratibu zikikamilika na wao wataweza kulipwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Nyakanazi -Rusumo pia Serikali ilishatenga fedha bilioni 3.8 na tayari bilioni tatu ilishalipwa, wananchi waliobakia ni 39 tu. Nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia na kwa sababu fidia hii imekamilika kwa zaidi ya asilimia 95, tutafuatilia kuhakikisha kwamba kidogo kilichobakia kinaweza kukamilika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tutaendelea punde, lakini kabla hatujaendelea nimeambiwa wageni wako wengi nje, kwa hiyo niwatangaze hawa waliopo ili wawape nafasi wageni wengine kuingia humu Bungeni.

Tutaanza na wageni waliopo Jukwaa la Spika, kwanza ni wageni tisa wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni viongozi wa *AMO Foundation* kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko ambao ni Walimu Wakuu wa Shule za Sekondari, Wakurugenzi na Wachungaji kutoka Tarime Mkoa wa Mara, karibuni sana. Hawa wameongozana pia na wageni 30 ambao ni walimu na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Tarime kutoka Mkoa wa Mara. Wanafunzi wako upande gani na walimu? Haya naambiwa wapo huku juu, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge nimeambiwa hawa walimu na hawa wanafunzi hapo wamefaulu sana. Kwa hiyo, niwapongeze walimu kwa kazi nzuri ya kuwasaidia wanafunzi kufanya vizuri. Pia niwapongeze wanafunzi kwa juhudi na bidii ya kuhakikisha mnafanya vizuri. Tunawatakia kila la kheri katika hatua nyingine huko mbele. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 36 wa Mheshimiwa Rose Tweve ambao ni viongozi wa Umoja wa Wanawake Tanzania kutoka Mkoa wa Iringa, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni 51 wa Mheshimiwa Dkt. David Mathayo ambao ni Viongozi wa Umoja wa Wanawake Tanzania, Wilaya ya Same, Mkoa wa Kilimanjaro, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge nikiwa nimesimama tuwe tunasikilizana, nikiwa nawaita majina kila siku haipendezi.

Tunao wageni 59 wa Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Mollel ambao ni wanafunzi na walimu wa Shule ya Msingi *Turkish Maarifa School* kutoka Arumeru, Mkoa wa Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 59 wa Mheshimiwa Anne Kilango Malecela ambao ni Madiwani, Wenyeviti na Katibu Kata Mwenezi kutoka Same Mashariki, Mkoa wa Kilimanjaro, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni 36 wa Mheshimiwa Anna Lupembe na Mheshimiwa Justin Nyamoga ambao ni Wanamaombi kutoka nchini Marekani, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni sita wa Msheshimiwa Edward Olelekaita ambao ni wawakilishi wa waliokopa matrekta kutoka Kiteto, Mkoa wa Manyara, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni watano wa Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, Taasisi ya Jicho la Tanzania kutoka Mkoa wa Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Nashon Bidyanguze ambaye ni jamaa yake kutoka Jijini Dodoma, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Khalifa Mohammed ambaye ni mtoto wake kutoka Newala, Mkoa wa Mtwara, Dkt. Mohamed Khalifa, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Benaya Kapinga ambaye ni mpigakura wake kutoka Mbinga, Mkoa wa Ruvuma, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wanafunzi nane na walimu 20 wa Shule ya Sekondari Benjamini Mkapa kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana Bungeni wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 71

**Fidia kwa wananchi waliochukuliwa maeneo yao na JWTZ**

**MHE. SUBIRA K. MGALU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itawalipa fidia wananchi wa Vijiji vya Msata, Kihangaiko na Pongwe Msungura kutokana na maeneo yao kuchukuliwa na Jeshi la Wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Stergomena Lawrence Tax, majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa vile na mimi ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu tangu niteuliwe tena kuwa Waziri wa Ulinzi na na Jeshi la Kujenga Taifa, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa baraka zake, lakini nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini kuendelea kumsaidia katika nafasi hii. Niahidi kwamba nitaendelea kufanya kazi zangu kwa uwezo wangu wote, kwa uaminifu, kwa uadilifu na kwa kujituma.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo, naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maeneo ya Vijiji vilivyotajwa yaani Msata, Kihangaiko, na Pongwe Msungura yapo katika Makambi mawili ya Jeshi ambayo ni *RTS Kihangaiko* na *Msata Military Training Base* katika Wilaya ya Chalinze. Serikali imeendelea na kutatua migogoro hii ya ardhi katika maeneo haya na katika mwaka 2021 ulifanyika uthamini wa awamu ya kwanza uliojumuisha Vijiji vya Msata, Pongwe Msungura na baadhi vitongoji katika Kijiji cha Kihangaiko. Uthamini awamu ya pili ulifanyika mwaka 2022 ukijumuisha vitongoji viiyosalia katika Kijiji cha Kihangaiko.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Uthamini uliofanyika mwaka 2021 iliwasilishwa katika Ofisi ya Ardhi Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze ili kukamilisha taratibu. Taratibu zitakapokamilishwa na Halmashauri ya Wilaya hii itawasilisha jedwali la malipo kwa Mthamini Mkuu wa Serikali kwa kuidhinishwa na hatimaye kufanyiwa uhakiki na malipo na Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, katika uthamini uliofanywa na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa mwaka 2022, Wizara ya Fedha imekwishafanya uhakiki kwa Vitongoji vya Funta, Chokozeni na Kudikongo, vilivyopo katika Kijiji cha Kihangaiko kwa ajili ya kulipa

fidia na malipo ya shilingi 330,788,467 yameshafanyika kwa wananchi katika Kitongoji cha Funta.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kushirikiana na Wizara ya Fedha, lakini pia na Halmashauri ya Chalinze ili kuhakikisha ulipaji wa fidia unakamilika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Subira Mgalu, swali la nyongeza.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza mawali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza niishukuru sana Serikali yetu ya Awamu ya Sita kwa kuonesha dhamira ya kushughulikia mgogoro huu ambao ulikuwa wa muda mrefu. Sasa kwa kuwa hatua ya kwanza ya kuanza kulipa malipo haya kwa Kitongoji cha Funta zaidi ya milioni 330 imeleta kama sintofahamu kwa wananchi wa Vitongoji vya Chokozeni na Kudikongo katika Kijiji cha Kihangaiko hicho hicho. Je, Serikali haioni ipo haja kwa vitongoji hivi viwili vya Kijiji kimoja cha Kihangaiko walipwe fidia yao kwa mwaka huu wa fedha unaoendelea?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa wapo baadhi ya wananchi waliotoa maeneo wa Vijiji vya Msata, Kihangaiko na Pongwe Msungura hawakupimiwa na kwa kuwa imeanza kulipa fidia. Je, Serikali inatoa tamko gani kwa wale wananchi ambao bado hawajapimiwa ili waweze kupata matumaini na waweze kuyaachia yale maeneo kuliko wanavyokwenda kufanya shughuli na wanakumbwa na matatizo makubwa? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kwa swali la kwanza ambalo ni kwamba kuna hawa ambao hawajalipwa, napenda tu kutoa rai kwa wenzetu ambao ni Halmashauri ya Chalinze kukamilisha taratibu na kuwasilisha jedwali ili taratibu ziendelee na ziweze kukamilika. Kama alivyosema ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba migogoro hii inakamilishwa na kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengi wataona tulikuwa na migogoro 87 katika mpango wetu wa

mwaka 2020 - 2023 na kati ya migogoro hiyo 87 migogoro 74 imekwishatatuliwa. Kwa hiyo hii 13 iliyosalia ni dhamira yetu kuhakikisha kwamba tunaikamilisha mwaka huu wa fedha kwani hata mpango tuliokuwa tumejiwekea kukamilisha mwaka 2023 umeshapita, tumeongeza mwaka mmoja.

Mheshimiwa Spika, kwa hao wengine ambao wamejitokeza, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaangalia kama hii migogoro mipya iko sehemu ya mpango wetu na kama haiko sehemu ya mpango wetu tutaona tunaiingiza namna gani. Jambo la kwanza ni muhimu tuende tukajiridhishe kwamba haya maeneo anayoyataja ni maeneo ambayo yapo katika maeneo ya vikosi vya Jeshi. Tutafanya hivyo Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na wewe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Alice Kaijage, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa vile changamoto iliyoko katika Halmashauri ya Chalinze inafanana na changamoto iliyoko katika Halmashauri ya Bagamoyo katika Kata ya Mapinga katika eneo la Kiharaka. Je, Serikali lina mpango gani kulipa wananchi wa eneo la Kiharaka katika Kata ya Mapinga? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishasema tunao mpango ambao umejumuisha migogoro mingi, kwa hiyo, kama hili eneo la Kiharaka ni sehemu ya mpango huu basi litakamilishwa katika mpango huu wa fedha, lakini kadri tulivyoendelea kutatua hii migogoro, migogoro mipya pia imekuwa ikijitokeza, kwa hiyo, kama huu ni mgogoro mpya tutaujumuisha katika mpango wetu

baada ya kujiridhisha kwamba ni eneo ambalo lina mgogoro na Jeshi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, moja kati ya maeneo ambayo yanaleta changamoto ni eneo la Kata ya Tambukareli ambapo ni eneo la Jeshi na kuna makaburi ya wananchi ambayo yapo kwenye eneo la Jeshi.

Je, Serikali mna mpango gani wa kwenda kufanya mazungumzo na wananchi ambao wamezika ndugu zao kwenye maeneo yale ili waweze kuendelea kufanya Ibada kwa marehemu waliotangulia mbele ya haki? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kuendelea kufuatilia suala hili kwa karibu sana. Hata kabla, huko nyuma tulishazungumza kuhusu suala hili, hili ni miongoni mwa maeneo ambayo yanafanyiwa kazi. Kwa hiyo, nikuhakikishie tu kwamba tutaendelea kulifanyia kazi ili tuweze kupata suluhu yake, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mbunge wa Mlimba, sasa aulize swali lake.

Na. 72

**Ujenzi wa barabara ya Mafinga – Mlimba**

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani kuhusu ujenzi wa barabara ya Mafinga hadi Mlimba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nami kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako kama Naibu Waziri wa Ujenzi, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, maana ametoa kibali hiki. Nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini ili niweze kumsaidia katika nafasi ya Unaibu Waziri wa Ujenzi, pia nikuahidi kwamba nitatoa ushirikiano wa hali ya juu kwa Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nijibu swali. Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mbunge wa Mlimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* imepanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara inayoanzia Mafinga, eneo la Kinyanambo 'C' hadi Kihansi (Mlimba) yenye urefu wa kilometa 126.39, ambapo katika mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya milioni 250 zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo. Baada ya kukamilika usanifu na gharama za ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, swali la nyongeza.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara ya Mafinga - Kihansi inaungana na barabara ya Ifakara – Mlimba - Madeke mpaka *Njombe Kibena junction,* ninaishukuru

Serikali kwa kuwa mwaka huu wa fedha bajeti ilitengwa ujenzi wa kiliometa 100 ianze kujengwa barabara hii ya Ifakara – Mlimba – Njombe, mpaka sasa taarifa nilizonazo mkataba umeshasainiwa ujenzi wa kilometa 62.5 uanze kujengwa. Swali langu dogo hapo ni kwamba; je, ni lini sasa mandarasi atakabidhiwa *site* na ujenzi uanze mara moja? *(Makofi)*

Kwa kuwa, barabara hii kwa mujibu wa bajeti ilitengwa kilometa 100 na kilometa 62.5 mkataba ulishasainiwa na kulikuwa na *Lot I* na *Lot II*. *Lot* zote mbili zilitangazwa mara moja. Swali langu la pili; je, hii *Lot II* kilometa 37.5 lini mkataba huu utasainiwa? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli *Lot I* kilometa 62.5 imeshasainiwa na Mkandarasi tayari alishapatikana na kazi hii imeshainiwa. Kinachosubiriwa sasa hivi, Mkandarasi baada ya kusaini anatakiwa atoe *performance guarantee* (dhamana ya utendaji) na lazima iwe imetolewa ndani ya siku 28. Kwa hiyo, tunaamini atakapokuwa amekamilisha takwa hilo la kisheria atakabidhiwa hiyo barabara ili aanze kufanya *mobilization* na inatakiwa ifanyike ndani ya siku 28.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara hii ni kweli kama alivyosema ni kilometa 100 *lot* mbili, hizi kilometa 37.5 ambazo zimebaki, tayari kila kitu kimekamilika tunachosubiri ni kusaini tu, hii ni pamoja na barabara nyingine ambazo zilikuwa zinasubiria utaratibu wakuzisaini. Kwa hiyo, tunaandaa utaratibu ili barabara hizo ziweze kusainiwa halafu wakandarasi waanze kuzijenga. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwa kuwa, barabara ya Mlowo –

Kamsamba iliingizwa kwenye bajeti kwa mwaka huu wa bajeti tulionao. Ningependa kujua ni lini Serikali itaanza kufanya kazi kwa vitendo, kuwaona wakandarasi *site?* Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara zote ambazo tumezitengea kuanza utekelezaji kwa mwaka wa fedha huu wa 2023/2024 ndiyo kwanza taratibu zinaandaliwa ikiwa ni pamoja na kuaanda *tender documents* ili ziweze kutangazwa, wakandarasi waombe na waweze kufanyiwa taratibu zote za manunuzi. Kwa hiyo, tupo kwenye taratibu za awali kwa sababu ndiyo tunaanza utekelezaji wa bajeti wa mwaka huu wa fedha, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ziwa Nyasa ni karibu wiki moja limechafuka na akina mama wajawazito wameshindwa kabisa kuvuka kwenda kupata huduma pale Matema. Je, Waziri yuko tayari sasa kufuatana na mimi kuangalia jinsi gani barabara ya kutoka Matema kwenda Ikombe inavyosuasua?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza tutoe pole kwa changamoto ambayo inatokea katika Jimbo la Kyela. Mheshimiwa Mbunge anafahamu kwamba yupo Mkandarasi ambaye alikuwa anasuasua na tayari tumeshamuagiza Meneja wa Mkoa wa Mbeya amsimamie ili kwanza aweze kukakamilisha eneo ambalo lilikuwa lina changamoto. Mimi nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya hapa tukubaliane tuende

tukatembelee ili kuhakikisha kwamba kazi ambayo inafanyika iweze kukamilika. Nipo tayari kufuatana naye.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, swali la nyongeza.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mtwara – Pachani – Luchili – Mkungu – Mtwara Matata – Ligera – Ligunga – Lusewa – Magazine – Lingusenguse – Nalasi – Mbesa mpaka Tunduru ina urefu wa kilometa 305, barabara hii ni ya kimkakati. Je, ni lini Serikali itaanza kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunatambua barabara hii ni kweli ni ya kimkakati na ya kiuchumi, tunachofanya sasa hivi, tulishakamilisha usanifu. Tulichoamua sasa hivi kutokana na urefu wa barabara na umuhimu wa hii barabara, tumeainisha maeneo yote ambayo yanasumbua pamoja na madaraja, tuyaimarishe na kujenga zege ama lami nyepesi ili barabara ile ipitike muda wote wakati huu tunatafuta fedha kuijenga barabara yote kwa kiwango cha lami. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kitonga ni barabara ambayo ni ya Kitaifa na imekuwa ikipitisha malori makubwa, inapopata ajali kidogo malori yamekuwa yakikwama kwa siku nzima au siku mbili, Serikali ilikuwa imetuahidi kujenga barabara mbadala ambayo itatokea Mahenge – Kudekwa kupita Wotalisoli mpaka Ilula.

Je, ni lini sasa ile ahadi ya Serikali itatekelezeka ili kuondoa changamoto kubwa katika Mlima Kitonga? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tuna kazi mbili ambazo tunazifanya, moja ni kuendelea kuipanua ile barabara ili iwe pana hasa hilo eneo la Kitonga, kuruhusu magari yaweze kupishana na kunapotokea changamoto tupate nafasi ya magari mengine kupita.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni kweli Serikali ina mpango wa kujenga *bypass* (njia ya mchepuko) kuchepusha kupita huo Mlima Kitonga kunapotokea changamoto na tumeunganisha nguvu kati ya *TANROADS* na *TARURA* ambao wanaendelea na usanifu wa hiyo barabara, baada ya hapo hiyo barabara itajengwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa.

Je, Serikali ina mkakati gani kukamilisha barabara ya Kiboroloni – Kichudini mpaka Kidia, kwa sababu barabara hii itakuwa inapandisha watalii kupitia Lango la Kidia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii ya Kiboroloni sasa hivi inasimamiwa na *TANROADS* kupitia Meneja wa Mkoa na imepangiwa fedha ya maendeleo kwenda kwa awamu. Sasa pengine tutaangalia ukubwa wake ili kama inawezekana tuweze

kuongeza fedha ili kipande kile kidogo kilichobaki kiweze kukamilika na ijengwe yote kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cosato David Chumi, swali la nyongeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Mwezi wa Sita tulisaini barabara ya Mafinga – Mgololo kupitia ule utaratibu wa *EPC+F*. Sasa wananchi wanapata shaka, wanasema mbona hawaoni mkandarasi, naomba Mheshimiwa Naibu Waziri awape *comfort* wananchi wa Mafinga katika barabara hiyo inayo - *cut across* Majimbo Matatu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI**: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa miradi yote ya *EPC+F* Wakandarasi walishapatikana na walishasaini mikataba ikiwa ni pamoja na hiyo barabara ya Mafinga kwenda Mgololo. Kinachofanyika sasa hivi ni kwamba Wakandarasi wote wapo wanapita *site,* moja ikiwa ni kuangalia fidia, kuangalia sehemu watakazopata *material*, wapi watajenga kambi lakini pia hizi barabara kutokana na ukubwa wake kuzigawa kwenye *lot* kulingana na mazingira yake watakavyogawa Wakandarasi maana yake atakayejenga siyo Mkandarasi mmoja kulingana na ukubwa wa barabara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kuna barabara ambazo zitakuwa na Wakandarasi wawili, hadi wanne kulingana na ukubwa. Kwa hiyo, Wakandarasi wako wanapita na kupitia pia usanifu kwa sababu ni wao pia wanatakiwa wajiridhishe na usanifu uliofanyika kabla ya kuanza ujenzi. Kwa hiyo, niwahakikishie wananchi kwamba mpango huo unaendelea na watu wapo kazini, kitakachofanyika baada ya kukamilisha wataanza kuona mitambo ikiwa inawasili kwenye maeneo yao, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam, swali la nyongeza.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Busisi – Sengerema hadi *Igaka boarder* ambayo inajengwa kwa barabara nne kwa kiwango cha lami. Lini kazi hiyo ya usanifu itaanza kufanyika maana yake toka imesemwa toka mwezi wa sita mpaka leo hatujamuona mkandarasi akifanya *designing*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tukishafanya usanifu kinachofuata ni kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza huo ujenzi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa Serikali imeshatoa *commitment* kwanza kufanya usanifu, basi hatua inayofuata itakuwa ni kujenga hiyo barabara kama ilivyosanifiwa. Kwa hiyo, mpango huo upo, hela zikishapatikana tutaanza kuijenga hiyo Barabara. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bonnah Kamoli, swali la nyongeza.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Spika, barabara ya Bonyokwa – Kinyerezi walisema itaanza mwezi wa sita mpaka sasa hivi hajiaanza, je, ni lini itaanza hiyo barabara? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba hiyo barabara tumeitengea bajeti kwenye bajeti ya mwaka huo wa 2023/2024 na kama nilivyosema kwenye barabara zingine ambazo zimepewa fedha kwa mwaka huu taratibu zipo zinaandaliwa ili zianze kujengwa ikiwa ni pamoja na hiyo barabara ya Bonyoka – Kinyerezi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaenda Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Salim Mussa Omar, Mbunge wa Gando, sasa aulize swali lake.

Na. 73

## *ATCL* kuanza safiri za Pemba

**MHE. SALIM MUSSA OMAR** aliuliza:-

Je, lini Shirika la Ndege Tanzania litaanza safari za Pemba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, majibu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kutujalia afya njema. Pili, kwa sababu ninasimama kwa mara ya kwanza hapa, nitumie nafasi hii kwa unyenyekevu mkubwa kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini na kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Uchukuzi. Kwa unyenyekevu mkubwa nimepokea uteuzi huu na ninaahidi kufanyakazi kwa juhudi, maarifa kwa ajili ya maslahi makubwa ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee ninakushukuru wewe kama mlezi na Kiongozi wangu kwa ushirikiano mkubwa ulionipatia nikiwa Msaidizi wako kwa nafasi ya Mwenyeketi wa Bunge na Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Kilimo na Mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, ninaomba sasa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi kujibu swali la Mheshimiwa Salimu Mussa Omar, Mbunge wa Gando, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *ATCL* itaanza safari za Pemba baada ya kupata ndege za kutosha kuweza kutoa huduma bila kuharibu ratiba za safari za sasa na urukaji kwa wakati. Kwa kuwa mwisho wa Septemba, 2023 *ATCL* inatarajia kupata ndege mpya moja aina ya *Boeing B737-9MAX* na ndege ndogo aina ya *Dash 8 Q300* matengenezo yake yanatarajiwa kuwa yamekamilika na kurejea katika ratiba zake za utoaji wa huduma. Uwepo wa ndege hizo kutaiwezesha *ATCL* kuanzisha safari zake katika kituo cha Pemba kwa tija na ufanisi mkubwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salim Mussa Omar, swali la nyongeza.

**MHE. SALIM MUSSA OMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali yenye kutia matumaini, lakini nimuulize swali la nyongeza.

Je, haoni kama ipo sababu ya kuweza kuweka kipaumbele au Wizara yake iko tayari kutoa kipaumbele kwa hili jambo ili kuweza kutatuliwa kwa haraka sana, kwa sababu Wapemba wanalaghaiwa na *issue* hii imekuwa kubwa sana. Sasa hivi ili Wapemba waweze kukupa dua ili uweze kutoboa katika mikeka ijayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Salim Mussa Omar kwamba Serikali inafahamu na inatambua uzito mkubwa na umuhimu wa kupeleka ndege hiyo Pemba na ndiyo maana imeshaanza mchakato. Alichokifanya ni kutukumbusha, nasi tutajitahidi kuongeza kasi zaidi ili angalau ndugu zetu Wapemba waweze kusafiri kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Martha Gwau, swali la nyongeza.

**MHE. MARTHA N. GWAU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi. Kwa kuwa Mkoa wa Singida ni jirani kabisa na Mkoa wa Dodoma ambao ndiyo Makao Makuu ya nchi: Je, ni lini Kiwanja cha Ndege Singida kitakamilika ili wananchi wa Singida wapate

huduma; lakini pia uwanja huo wa Singida utumike kama uwanja wa dharura kama Dodoma kuna changamoto? Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

Aah, Mheshimiwa Naibu Waziri, naona aliyekuwa pacha wako kipindi cha nyuma, sasa hivi ni mwingine. Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi anataka kusaidia hapo kujibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Singida ni mkoa ambao uko karibu na Dodoma na Serikali tayari imeshafanya usanifu wa Uwanja wa Singida ili uweze kujengwa, kwani unaweza ukatumika sana pale ambapo kunatokea changamoto katika viwanja vya Mkoa wa Dodoma, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, naona unanitazama, labda unalo la nyongeza la kusema, karibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi kwa kunisaidia. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya usanifu kukamilika, hatua inayofuata sasa ni kujua mahitaji halisi kwa ajili ya fidia ili hatimaye tuweze kuanza kufanyia kazi huo uwanja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi. Serikali ndivyo inavyopaswa kufanya kazi. Tunarajia muwe mnasikiliza majibu, kwa sababu ninyi mnatakiwa kujibu. Kama wewe unalijua la ziada, basi inarahisisha. Kwa hiyo, nakupongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi

kwa majibu hayo uliyoyatoa kwa swali la Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wako wageni walioingia hapa ndani baada ya kutangaza wageni wengine waliokuwa wametangulia.

Tunao wanafunzi 140 na walimu watano kutoka Shule ya Sekondari ya Wasichana ya *St. Christina* ya Jijini Tanga. Haya, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaleta matangazo mengine niliyonayo hapa mbele, leo asubuhi wakati tukianza shughuli zetu kabla ya maswali, kama sehemu ya Orodha za Shughuli za Leo iliwekwa Taarifa hapa mezani na Kamati yetu ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo. Sasa nataka kuizungumzia hiyo halafu nilete matangazo mengine yaliyo hapa mbele.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kuwa siku ya Alhamisi, tarehe 13 Aprili, 2023 kwenye Kikao cha Sita, Mkutano wa Kumi na Moja, Bunge lilijadili Hoja ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Wakati wa mjadala kuhusu hoja hiyo ilijitokeza suala la changamoto za utekelezaji wa Mkataba wa Ukopeshaji wa Matrekta ya Kampuni ya URSUS.

Waheshimiwa Wabunge, suala hilo lilijadiliwa kwa hisia kali miongoni mwa Wabunge waliokuwa wakiwasemea wananchi ambao waliathirika kutokana na mkataba huo. Kufuatia hali hiyo nilimuagiza Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kukutana na Wabunge wa maeneo yaliyokuwa na wananchi waliothirika kiasi kikubwa ili kuwasikiliza na kubaini ukubwa wa tatizo. Nilimtaka Mwenyekiti wa Kamati hiyo kunijulisha matokeo ya kikao hicho ili tupate kulielewa suala hili kwa undani na kuona namna itakayofaa ya kulishughulikia.

Waheshimiwa Wabunge, Mwenyekiti wa Kamati alikutana na Wabunge hao kama nilivyoagiza na aliwasilisha kwangu

taarifa iliyokuwa na mapendekezo kutokana na mkutano baina yake na Wabunge hao. Kwa kuzingatia taarifa hiyo ya awali niliona umuhimu wa suala hilo kufanyiwa kazi na Kamati nzima na kisha kuwasilisha kwangu taarifa ya matokeo ya kazi hiyo ikiwa ni mapendekezo ya kutatua changamoto zilizopo.

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 20 Aprili, hapa nadhani tarehe imekosewa kidogo, lakini katika kikao hicho hicho cha Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge niliielekeza Kamati kushughulikia suala hili na kuwasilisha taarifa Bungeni wakati wa kipindi cha siku sita za majumuisho ya Bajeti kwa mujibu wa Kanuni ya 124 ya Kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka 2023 ili kuipa Kamati malengo maalum niliipatia hadidu za rejea zifuatazo:-

(a) Kuchambua mikataba inayohusika katika mradi wa matrekta ya Kampuni ya URSUS yaliyokopeshwa kwa wakulima ili kulinganisha matarajio ya wakulima na Serikali kwa ujumla na matokeo halisi ya utekelezaji wa mikataba hiyo;

(b) Kubainisha changamoto za kiutendaji katika mikataba ya mauziano ya matrekta ya Kampuni ya URSUS;

(c) Kutathmini utaratibu wa malipo ya fedha za marejesho ya mikopo ya matrekta kutoka kwa wakulima kwenda kwa mkopeshaji;

(d) Kubainisha na kushauri kuhusu utaratibu bora unaoweza kutumika katika kutatua changamoto zilizobainika; na

(e) Kushughulikia jambo lingine lolote linalohusiana na mkataba huu litakalobainika kuwa na tija katika shughuli hii ya Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, Kamati ilifanya kazi yake ikiwemo kukutana na mamlaka mbalimbali za Serikali kwa lengo la kuchunguza na kubaini uhalisia wa jambo hilo. Wakati Kamati ikiendelea na majadiliano kati yake na Serikali yapo mambo

yaliyojitokeza na kunifanya niamue kwamba badala ya taarifa hii kuwasilishwa kipindi cha majumuisho ya Bajeti iwasilishwe wakati mwingine.

Waheshimiwa Wabunge, Kamati imekamilisha kazi yake na kuwasilisha taarifa kwangu na nimeisoma kwa ukamilifu. Taarifa hiyo imewasilishwa mezani leo kama mlivyoona, kwa ujumla pamoja na mambo mengine taarifa hii inabainisha kwamba malalamiko ya wakulima kuhusu hali mbaya ya matrekta ya URSUS ni ya msingi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mtazamo huo umethibitishwa na maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati na mamlaka mbalimbali zilizokutana na Kamati ikiwemo Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC)*.

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na changamoto za utekelezaji wa mkataba wa mauziano ya matrekta ya Kampuni ya URSUS, wakulima wa sehemu mbalimbali waliohusika katika mradi huu waliathirika kwa namna tofauti; wapo waliopata hasara kutokana na kuuziwa matrekta yasiyo na ubora ama yenye viwango duni na kuwagharimu baadhi yao kuuza mali zao na hivyo kurudisha nyuma juhudi zao za kuondokana na umaskini; na wengine waliathirika kiasi cha kuuza mali zao na kuingia kwenye migogoro na familia zao na kusambaratika familia hizo.

Waheshimiwa Wabunge, Kamati imeonesha kuwa katika athari hizo wapo wananchi waliweza kulipa deni japo kwa shida na wengine kubaki na hali ngumu za kiuchumi; lakini pia wapo wengine hawajamaliza madeni yanayowakabili kwa kukopa matrekta na kuendelea kukabiliwa na mzigo wa gharama za matengenezo ya matrekta hayo yasiyo na ubora kama ilivyobainishwa na Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, kwa ujumla zimebainika changamoto za kiutendaji ambazo zinahitaji kupatiwa ufumbuzi ili kutoa unafuu kwa wananchi hao, kwa mfano, nilipoipitia Taarifa ya Kamati nimeona imebainisha kuundwa kwa timu ya Serikali ya majadiliano tangu mwaka 2019 ambayo hadi Kamati inakamilisha

kazi timu hiyo haikuwa imemaliza kazi yake, wala kutoa mrejesho wowote.

Waheshimiwa Wabunge, tunaona kuwa hii ni changamoto ya wazi na kwa hiyo, inahitaji kufanyiwa kazi kwa sababu hiyo ni miaka takribani minne sasa tangu timu hii ianze kazi yake na haijamaliza kazi hyo.

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na maelezo hayo nimeamua kama ifuatavyo:-

(a) Kwanza Serikali ichambue na kubainisha makundi mbalimbali ya wakulima walioathirika kutokana na mradi huo wa kuwakopesha matrekta ya URSUS na kuonesha namna ya kuwapatia nafuu waathirika hao. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hoja hii inatokana na kwamba yale makundi yaliyo mbalimbali lipo kundi ambalo limeshamaliza kulipa yale madeni, lipo kundi ambalo limelipa kwa sehemu na lipo kundi ambalo halijaanza kabisa kulipa madeni hayo, na hiyo inatokana na kwamba hawakupewa matrekta yanayofanana, zilikuwa ni aina mbalimbali, kwa hiyo, kuna makundi pia ya aina za matrekta walizopewa na kwa hiyo, hayo nayo ni makundi mengine kadhaa, na vivyo hivyo waliingia mikataba ambayo haifanani, mikataba inatofautiana kutoka kundi moja mpaka kundi lingine na kwa hiyo, mfumo pia wa marejesho unatofautiana kutoka kundi moja kwenda kundi lingine, na kwa hivyo hivyo wale wakulima walivyo kwenye makundi kuna makundi hayo pia yanayoonesha ni kiasi gani cha pesa kimelipwa kwa wale ambao wameshakamilisha, lakini wale ambao bado na wenyewe wapo kwenye makundi mbalimbali na wale ambao hawajalipa kabisa nao wamegawanyika hivyo. Kwa hiyo hilo agizo linazingatia taarifa hii ambayo nimeletewa na Kamati.

(b) Timu ya Serikali ya majadiliano iliyoundwa ikamilishe kazi yake na kutoa mrejesho inavyopaswa ili Serikali ifikie hatua nyingine ya kuwakwamua wakulima walioathirika.

(c) Taarifa zote zilizotakiwa na Kamati bila kupatikana ziwasilishwe kwa Katibu wa Bunge kabla ya kipindi cha Vikao vya Kamati vya mwezi Oktoba, 2023 ili Kamati izifanyie kazi. *(Makofi)*

Taarifa hizo ni pamoja na:-

(i) Ripoti ya Ukaguzi uliofanywa na Kituo cha *CARMATEC* na kubainisha dosari kwenye matrekta ya URSUS;

(ii) Ripoti ya makabidhiano ya mradi kutoka SUMA-JKT kwenda *NDC*; *(Makofi)*

(iii) Ripoti ya kikao cha timu ya Serikali ya majadiliano *(Government Negotiating Team); (Makofi)*

(iv) Ripoti ya Wizara ya Fedha kuhusu malipo ambayo yamekwisha kufanyika; *(Makofi)*

(v) Ripoti ya TAKUKURU kuhusu ushiriki wake katika utekelezaji wa mkataba huo; na *(Makofi)*

(vi) Ripoti ya Kampuni ya Udalali ya *Majembe Auction Mart. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na maagizo hayo mahsusi, ninaikabidhi kwa Serikali taarifa yote ya Kamati iliyowekwa mezani mapema leo hii.

Baada ya kuipokea Serikali iyafanyie kazi mapendekezo yote ya Kamati pamoja na maagizo hayo mahsusi, kisha Serikali iripoti kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo. Kamati hii ifuatilie kwa karibu utekelezaji wa Serikali kuhusu utatuzi wa changamoto hii na kuripoti kwenye taarifa yake ya mwaka wakati wa Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge, yaani mwezi Februari, 2024. *(Makofi)*

Kwa kuzingatia kuwa changamoto zinatofautiana kwa kundi moja lililoathirika hadi lingine, ni dhahiri yapo majibu ya utatuzi wa migogoro ambayo yatakuwa ya muda mfupi na mengine ya

muda wa kati na mengine ya muda mrefu. Kamati itakuwa inatoa taarifa kuhusu changamoto hii ya matrekta ya URSUS kwenye taarifa zake za Januari-Februari lakini pia kwenye taarifa zake za kipindi cha Bajeti.

Kwa hiyo, tunatarajia kwamba taarifa hizo za Bunge zitakapokuwa zinaletwa hapa zitakuwa na kipengele mahsusi kuhusu utekelezaji wa haya ambayo Bunge linaiagiza Serikali na mwishoni tutafika mahali ambapo hata yale ya muda mrefu Serikali itaweza kuieleza Kamati inajipanga vipi kuwasaidia wakulima waliopata athari kubwa kwa kupata matrekta haya ambayo nia ilikuwa njema, lakini hiyo nia njema imeenda kuwa mzigo kwa wakulima waliopata matrekta hayo.

Waheshimiwa Wabunge huo ndio uamuzi wangu baada ya kuipitia taarifa hii ya Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo. *(Makofi)*

Kwa namna ya kipekee nitumie nafasi hii kuwashukuru sana Kamati yetu ya Kudumu ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kushughulikia changamoto hii ambayo wakulima wetu wameipata na kwa hivyo kipekee nimshukuri sana Mwenyekit wetu, ama anaweza kuitwa sasa aliyekuwa Mwenyekiti wetu Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile kwa kazi nzuri aliyoifanya kuhusu changamoto hii ama kadhia hii ambayo wananchi wameipata na pia tunakutakia kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yako mapya kama Naibu Waziri wa Uchukuzi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia nitumie fursa hii kumshukuru Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Mariam Ditopile kwa kuendeleza jambo hili mpaka tumefika sehemu hii na pia niwashukuru Wajumbe wote wa Kamati hii kwa ushirikiano mliouonesha katika kipindi cha muda mfupi mmeweza kuzitafuta taarifa zote hizi na kubainisha changamoto zilizopo, lakini pia kutoa mapendekezo mbalimbali ili Serikali iweze kuyafanyia kazi hayo na kuona namna ambavyo inaweza kutatua changamoto hii ambayo imewapata wakulima. *(Makofi)*

Kwa upande wa Serikali nawatakia kila la heri katika utekelezaji wa maagizo haya ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, nilete tangazo lingine ama matangazo mengine; kwanza Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* anawatangazia Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya *Bunge Sports Club* pamoja na makepteni wa timu zote kuwa leo tarehe 4 Septemba, 2023 kutakuwa na kikao kwenye ukumbi namba 229 Jengo la Utawala mara baada ya kuahirisha Bunge hapa, kwa hiyo mnaombwa muende huko na Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club.*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine ni taarifa ambayo inaeleza mambo yaliyojitokeza kwenye *NMB Bunge Bonanza* lililofanyika Jumamosi tarehe 2 Septemba, 2023 kwenye Shule ya Sekondari ya John Merlin – Miyuji Dodoma.

*NMB Bunge Bonanza* lilifanyika Jumamosi tarehe 2 Septemba, 2023 likishirikisha Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini pia na Wawakilishi 10 kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar, watumishi wa Ofisi ya Bunge pamoja na watumishi wa Benki ya *NMB* ambapo Benki ya *NMB* walikuwa wadhamini wakuu wa *Bonanza* hilo lililobeba kauli mbiu ya "Shiriki Michezo Jenga Jamii yenye Afya." Mgeni Rasmi alikuwa Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid.

Waheshimiwa Wabunge, *bonanza* hilo lilihusisha michezo mbalimbali kama mpira wa miguu, mpira wa pete, mpira wa kikapu, kufukuza kuku, kupenya kwenye pipa, bao, drafti, karata, kula chakula na soda kwa haraka na kadhalika. Matokeo ya michezo; kwanza michezo ya timu; mpira wa miguu Wabunge walishinda magoli matatu kwa sifuri, nikawa nafikiri wamefikisha matano kama Yanga, lakini kumbe hayakufika. *(Makofi)*

Haya mpira wa pete watumishi walishinda seti 22 kwa 12; mpira wa kikapu wanaume Wabunge walishinda seti 25 kwa 20; mpira wa kikapu wanawake Wabunge walishinda seti 16 kwa 14; mpira wa wavu wanaume watumishi walishinda seti mbili kwa

moja; mpira wa kikapu wanawake Wabunge walishinda seti mbili nafikiri kwa moja. *(Makofi)*

Washindi wa medali, washindi wa kwanza wa kila mchezo wa mtu mmoja mmoja walipewa medali ya dhahabu kwa upande wa Wabunge ni hawa wafuatao; karata Mheshimiwa Hawa Mwaifunga; bao Mheshimiwa Issa Mchungahela na Mheshimiwa Maimuna Mtanda; drafti Mheshimiwa George Mwenisongole na Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza; kurusha tufe wanawake Mheshimiwa Tamima Haji Abass; kukimbia na gunia Mheshimiwa Simai Hassan; kunywa soda kwa haraka Mheshimiwa Francis Isack; kula chakula kwa haraka Mheshimiwa Issa Mtemvu; kukimbia na glasi yenye maji Mheshimiwa Francis Isack na Mheshimiwa Stella Fiyao; kuruka kwa urefu wanawake Mheshimiwa Felista Njau; kukimbia na yai kwenye kijiko, Mheshimiwa Festo Sanga na Mheshimiwa Ally Makoa; mpira wa meza Mheshimiwa Frank Isack. *(Makofi)*

Samahani hapa wamekosesa huyu ni Mheshimiwa Francis; mpira wa meza Mheshimiwa Francis Isack; *pool table* Mheshimiwa Hassan ambaye huyu ni anatoka Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Michezo ya riadha mita 100 wanawake, Mheshimiwa Hadija Pande Juma anatoka Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Washindi wa jumla kwenye *Bonanza* hilo walikuwa ni timu ya watumishi wa Bunge waliopata alama 121 dhidi ya Waheshimiwa Wabunge waliopata alama 112. Taarifa imetolewa na Makamu Mwenyekiti wa *Bunge Bonanza* huyu ni *CPA* Layson Mwanjisi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi kwa kukubali kuja kuwa Mgeni Rasmi kwenye bonanza letu hili na amekuja hapa na ametuahidi kwamba na yeye ataenda kufanya hivyo kwa hiyo bila shaka Wabunge tutakuwa tayari kwenda kushiriki pia michezo Zanzibar na pia niwapongeze Wabunge wote mliofanya vizuri katika michezo hii na wale wenzangu na mimi basi tujitahidi siku nyingine na sisi tushiriki na tufanye vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo kwa kuwa shughuli tulizokuwa nazo leo tumekamilisha naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 6.00 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 5 Septemba, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*